


# SAUTI ISIYOJULIKANA

 Asante sana, Ndugu, Mungu akubariki. “Mwanangu, Timothy.” Hilo ni zuri sana. Mungu akubariki. Hujui jinsi hilo linavyonifanya nijisikie, kumwona kijana mwanamume, kusikia maneno hayo, yakisemwa namna hiyo. Inamaanisha, Ndugu, kwamba kazi yangu haikuwa bure. Ninazidi kuzeeka, naye ndiye anayefuata nyayo. Na sasa, inanifanya tu nijisikie vizuri sana kusikia mkutano kama huo, kile ulicholeta. Kamwe hujui unachofanya wakati unapopanda Mbegu.

<sup>2</sup> Kuna hekaya huko Norwe kwamba, wana maua mengi mazuri Norwe, nayo hekaya ni, kama John Appleseed hapa, mwajua, kwamba mtu huyu alipenda maua vizuri sana hata alijaza mifuko yake mbegu, naye akazunguka akipanda tu mbegu. Kila mahali angeona mahali fulani, alipanda mbegu za maua, na hiyo ndiyo sababu kuna maua mengi sana, kwa sababu mtu fulani alipanda mbegu. Jambo ndilo hilo.

<sup>3</sup> Hebu na tupande Mbegu ya Neno la Mungu popote tulipo, kwa kuwa hatujui yale litakayozaa. Na hizo Mbegu chache, usiku huo, zilianguka kwenye udongo wenye rutuba ambao huzaa mtumishi ha—halisi wa Mungu, akisimama hapa kama nuru inayoangaza.

<sup>4</sup> Nilipitia karibu na kanisa lake hivi majuzi, wala simkumbuki huyo mvulana, bila shaka, lakini, kwangu mimi yeye ni mtoto tu, nina shaka kama ana umri kama wa Billy wangu. Lakini yeye ni...Nikisimama kule, nikiona kanisa hili zuri, kubwa la Assembly of God lililojengwa kule chini, nilisimama kwa dakika moja tu, nikasema, “Asante, Baba, dumisha mkono Wako juu yake.”

Na, tunapoachana, tunaacha nyuma yetu  
Kumbukumbu za kudumu.

Hakika ni sikukuu ya furaha, yenye furaha sana ya ukumbusho. Baraka za Mungu juu yenu nyote.

<sup>5</sup> Sasa, kesho ni Jumapili, nasi tunawatarajia ninyi wageni wote kuhudhuria kanisa la mtu fulani kesho. Watu hawa hapa jukwaani ni watu ambao ni wahudumu wa huku, nao wako hapa wakiwakilisha Injili hii ambayo mnatusikia tukihubiri. Wanaamini jambo lile lile tunaloamini, nao wameketi hapa wakiiwakilisha. Basi yajazeni makanisa yao kesho, mwe na wakati mzuri sana.

<sup>6</sup> Halafu basi, kesho alasiri, tunafanya ibada ya alasiri, badala ya kuwa na ibada ya jioni, kwa sababu inawavuta tu watu kutoka kwenye wajibu wao wenyewe, basi tunaweza kuifanya alasiri. Tunapaswa kuabudu Jumapili siku nzima, hiyo ndiyo

siku iliyotengwa kwa ajili ya hilo. Kwa hiyo sasa, hudhurieni shule ya Jumapili asubuhi, mahali fulani, kisha mlingojee kanisa.

<sup>7</sup> Na daima ni dhambi kuwatuma watoto wenu kwenye shule ya Jumapili, mnajua hilo, kila mtu anajua hilo. Ni dhambi kuwatuma watoto wako kwenye shule ya Jumapili, wapeleke. Hiyo ni . . . Kwa hiyo basi, mnatenda mema, lakini mnafanya makosa kwa kuwatuma tu.

<sup>8</sup> Halafu basi, kesho alasiri, saa nane na nusu, iweni hapa kwa wakati mzuri mkiweza. Nasi tunatarajia ibada nyingine ya uponyaji kesho alasiri. Ninaomba Bwana atatupa kwa wingi sana, kesho alasiri. Imekuwa ibada nzuri sana!

<sup>9</sup> Kama hao . . . kama mpishi huyo ama mpishi huyo mkuu aliyepika kiamshakinywa hicho asubuhi ya leo, hapa kwenye ninii, sijui tunavyopaita mahali hapo kwenye eneo hili hapa, aisee, hicho kilikwa ni kizuri kweli. Kwa kweli, huo ndio mlo wa kwanza mzuri, mgumu ambao nimekula juma hili. Nao . . . Hizo biskuti ama mkate, chochote kile, mkate mtamu, huo ulikuwa mzuri, kamwe . . . Ni—niliupenda huo kweli. Ningependa kupata mapishi hayo. Dada Wood, wewe yapelekee Meda nyumbani, uone kama angeweza kujaribu kuyapika. Huo ni upishi mzuri wa Kimethodisti, huo kweli ndio . . . ulikuwa mzuri kweli. Tunauthamini huo.

<sup>10</sup> Na kama ikitokea kwamba paroko yupo, tunasikitika kwamba tulikaa muda wa ziada, bila kujua. Bila shaka nasikia, Ndugu, bwana, kwamba—kwamba labda ibada zenu, ninyi nyote hupangia ibada zenu muda *fulani*, na mmezoea hilo moja kwa moja. Lakini nawaambia, Ndugu, hawa Wapentekoste kweli huwa na yubile ya ulaji wanapokuja huku, nao wanakaa tu siku nzima, inakubidi tu kuwafukuza, hakuna lingine, unawaondoa tu—unawaondoa mikononi mwako. Kwa hiyo wao . . . Lakini tulijaribu kufumukana, Billy aliashiria dakika kumi na tano, nami nafikiri tuliumaliza kabla ya dakika kumi na tano kwa ajili yenu. Nasi tunasikitika kwamba tulikatiza pale, kwa sababu hatukujua hilo.

<sup>11</sup> Na bila shaka tunawashukuru, kutoka kwenye vilindi vya moyo wetu, kwa kuturuhusu tupate hicho kiamshakinywa. Nanyi wanawake wazuri mliohudumu, na chochote kile, asanteni sana. Baraka nyingi za Mungu ziwe pamoja nanyi.

<sup>12</sup> Sasa, nilikuwa nikiwazia, siwezi kuliondoa mawazoni mwangu, juu ya huu, wongofu wa Ndugu Hill. Ndugu Banks Wood, mmoja wa wenzangu, ameketi hapa, usiku wa leo, mahali fulani, nadhani hakwenda nyumbani leo, lakini alikuwa mkutanoni asubuhi ya leo. Hapo ndipo mvulana wake, kweli, ule mkutano kabla tu ya huyo kuponywa. Kila wakati anapotaja mkutano, mimi . . . jambo zuri sana. Sasa, ningetaka tu, sitaki kuondoka kwenye somo langu hapa, lakini ningetaka tu

kusimulia jambo dogo lililotukia ambalo lilinikera sana kwenye mkutano huo; ule ule ambamo uliongokea.

<sup>13</sup> Nawaambia, jinsi ilivyo rahisi kuondoka tu kwenye Ufalme wa Mungu, usiponini. . . Maskini mama yangu alikuwa akiniambia, akasema, “Mpenzi, sikuzote wazia mara mbili, na ndipo unene mara moja.” Hiyo ni falsafa nzuri sana, sana, ni nzuri kweli.

<sup>14</sup> Nilikuwa nikiishi, kama mjuavyo, mkutano ulikuwa mzuri, nasi tulikuwa tukikaa huko mashambani. Kulikuwa na madoido mengi mkutanoni wakati huo, kumetulia pakubwa tangu wakati huo, kwa sababu, loo, Oral Roberts, na wengine wengi wameingia hudumani, kwa hiyo wao. . . Ni. . . Uamsho Marekani karibu umekwisha, mnajua hilo, tunaokota tu masazo sasa, mahali tu ambapo, karibu yote yamekwisha sasa.

<sup>15</sup> Nami nafikiri. . . Hiyo ndiyo sababu ninaonya kwa moyo wangu wote, “Hukumu italifuata hili, hakika kabisa.” Hapajawahi kuwa—hapajawahi kuwa na wakati wowote katika historia, pasipo kufuatwa na hukumu, nayo hukumu italifuata hili. Nao uamsho wa uponyaji karibu umekwisha Marekani sasa. Nao moyo wangu unatamani kwenda ng’ambo, ambako, labda katika miezi michache, huenda nikafanya ninii yangu, ninii yangu iliyosalia, nikae katika nchi za kigeni maishani mwangu mwote.

<sup>16</sup> Sasa, kwa hiyo, katika mkutano huu ilinibidi kukaa huko mashambani, nami nilikuwa kwenye moteli ndogo, huenda ikawa huyo ndugu anajua, kama anatoka sehemu hiyo ya nchi. Basi kulikuwa na mkahawa mdogo, naamini ulikuwa ni mkahawa wa Kimenoni upande wa pili wa ba—barabara, nao walikuwa. . .

<sup>17</sup> Sasa, Wamenoni ni watu wazuri kweli. Nilipita leo na kuona hospitali ya Wamenoni hapa mjini, kama ningevunjika mkono na kulazimika kwenda hospitalini, natumaini watanipeleka kwenye hospitali ya Wamenoni, maana ni—ninawapenda watu hao, ni wazuri kweli. Nao wanakupa kila mara, ninaamini ni ninii. . . Gene, kuna wakia ngapi katika ratili? Kumi na sita, sivyo? Wanakupa kumi na saba. Mnaona? Na kwa hiyo, basi ni watu wazuri kweli.

<sup>18</sup> Nami nilikuwa kwenye huo mkahawa, na maskini wanawake hao wamevalia vizuri sana, safi, na meko yao yalikuwa safi, nao walikuwa nadhifu, wanawake wazuri, kwa kila hali ni mama Mkristo halisi. Nami kweli nilifurahia kula huko, chakula chao kilikuwa kizuri, na kwa hiyo ningeenda huko na kula.

<sup>19</sup> Vema, Jumapili sikuwa nimekula labda kwa siku mbili, nikijiandaa kwa ajili ya ibada kuu ya alasiri, labda wakati mvulana huyu alipoongoka, ama, kuletwa kwa Kristo. Na kwa hiyo, Bw. Baxter alikuwa akizungumza kwa niaba yangu, kama mnakumbuka, ibada za alasiri katika—katika

matangulizi. Na kwa hiyo, ni—nikaona njaa, nami nilijua nilikuwa ninaenda tu kuhubiri alasiri hiyo, sikuwa nifanye ibada ya uponyaji, kwa hiyo kidogo niliwaza, “Vema, isingenidhuru kula sambusa.” Nikasema, “Ni—ninahubiri kwa nguvu sana, kwa kawaida,” nikasema, “na kwa muda mrefu sana, cho—chote kitameng’enywa kabla usiku wa ibada ya uponyaji kufika.”

<sup>20</sup> Kwa hiyo nikasema... Nikaenda kule, na mahali hapo padogo pa Menoni palikuwa pamefungwa, nao walikuwa wameenda kanisani, na mahali hapo palikuwa pamefungwa. Kwa hiyo nikavuka barabara mpaka kwenye kituo kidogo cha kawaida cha Marekani, ambapo walikuwa na sambusa na vinywaji baridi.

<sup>21</sup> Ninachukia kusema jambo hili, linaniumiza tu, maana ni taifa letu wenyewe, bali kuliona linadhaliika hivi! Nilipoingia mahali hapo, kitu cha kwanza kilikuwa ni polisi, amesimama huku amemkumbatia mwanamke mahali pabaya, akicheza mtambo wa karata. Sasa, kucheza karata ni haramu Ohio, wengi wenu enyi watu wa Ohio mnajua hilo. Halafu polisi, anayepaswa kuwa analinda sheria, amesimama pale akiivunja hiyo sheria, na ni mwanamume wa rika yangu, labda alikuwa na watoto nyumbani, na mke, amesimama pale amemkumbatia mwanamke. Nikaangalia, nikawaza, “Loo, jamani!”

<sup>22</sup> Nikamsikia mtu fulani akicheka, nikaangalia nyuma, na kundi la hawa wavulana hapa... Mnawaitaje? Wahuni, ama chochote kile...? Hizo hapo nywele zilizokatwa kibapa juu, na bata ameketi nyuma ya shingo yao ama chochote kile, wamevaa jaketi za ovaroli, na suruali zao zimevutwa chini namna *hii*, na... Enyi wavulana, kuwa mwanaume. Mna mwaumbile mazuri kuliko hayo. Jamani! Kwa hiyo hao hapo wameketi huko nyuma, na msichana mdogo, asiyezidi umri wa miaka kumi na saba au kumi na minane, na huyo msichana, jinsi walivyokuwa wakifanya, akimvuta kwake, ilikuwa ni aibu. Nami nikawaza, “Vema, vipi kuhusu hilo?”

<sup>23</sup> Nikasikia mtu fulani akisema, “Unafikiri mvua itadhuru rubabu?” Nikaangalia upande *huu*, na hapo aliketi mwanamke, Ni—ninasema... Si—sininii—siamini hapa ni mahali pa kufanyia mzaha, hapa ni mahali pa kuwa mwaminifu na mkweli. Basi hapo aliketi mwanamke ambaye angeweza kuwa ni nyanya yangu. Alikuwa ameketi hapo amevaa hizo nguo fupi sana za kizinifu, naye huyo mwanamke alikuwa na makucha yaliyopakwa rangi ya zambarau. Sasa, nimekuwa na ukucha wa zambarau, lakini ni baada ya kujikwaa, ama chochote kile, bali zilikuwa kucha za miguu zilizopakwa rangi ya zambarau, pamoja na rangi ya *vidole* ya zambarau midomoni mwake, mwajua, na—na—na madoa madogo usoni mwake. Na maskini... huyo mama alikuwa na nywele zilizokatwa fupi sana, na kupakwa rangi ya samawati.

24 Sasa, mimi—mimi. . . Huyo, sasa, mama huyo ana haki ya kufanya chochote atakacho, mnaona, hilo si kitu kwangu, mnaona, lakini si—siamini Bwana aliwahi kumfanya mtu yeyote mwenye nywele za bluu. Mimi—mimi. . . Ilionekana ya kigeni sana. Ndipo maskini huyo mama, mkongwe, na nyama mkononi mwake zilizolegea, zikining'inia, mwajua, namna *hiyo*. Na kwa hiyo, nikamwangelia.

25 Na kulikuwako na mzee, na ilikuwa, ninahofia ulikuwa umeenda sana, msimu wa kiangazi, mwishoni mwa majira ya kuchipua, yapata Mei au Juni, huku maskini jamaa huyo ameketi pale amevaa koti kubwa la jeshi, na skafu kubwa imezungushiwa shingoni mwake, mbili, amelewa. Walikuwa wameketi pale, wakinywa. Kwa hiyo, wakaomba radhi wakaondoka, wakamwacha huyo mwanamke peke yake.

26 Nikasimama pale, nami nikasema, “Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, nimetoka kwenye kilele cha mlima nikaja kwenye tundu la panya.” Kisha nikasema, “Waweza je Wewe, ukiwa mtakatifu, jinsi ninajua ndivyo ulivyo, kamwe kuangalia mandhari kama hiyo, na kuacha iwepo? Kwa nini usitume tu tetemeko la ardhi na kuzamisha kitu hicho chote?” Nikasema, “Kumaanisha kwamba itabidi maskini mtoto wangu Sarah na Rebekah walelewe chini ya upuuzi kama huo! Iwalazimu, kama msichana yule kule nyuma, na hebu angalia hapa kwenye hilo, wanawake, na hapa, na wanaume wakitenda jinsi wanavyotenda! Nazo sheria za nchi yetu zimeoza na kuchafuka, na—na. . .” Hizo sheria ni sawa, lakini wale wanaojaribu kuzitekeleza, na kitu kama hicho! Nikawazia. . .

27 [Dada mmoja ananena kwa lugha, ndugu fulani anafasiri: “Naam, mngepata nini ila upendo wa Mungu? Naam, nawaambia, usiku wa leo, watu wangu, amkeni, naam, kwa kuwa Mimi ni Mungu wala sitavumilia hilo, naam, hawatavumilia, asema Mungu. Hivi sitafanya, kama asemavyo? Naam, je, nabii Wangu hatawaletea mambo ya usoni? Naam, na je, sitasema nanyi, na kusema ya kwamba hakika utaangamia usipoimarishwa? Naam, nasema, wewe ndiwe utakayesema yatakayotendeka. Hata hivyo, ninasema ni Mimi, Mungu, atakayetwaliwa, naam, ni Mimi, Mungu atakayetolewa kwenu. Naam, kisha nasema, mkubalini, usiku wa leo, tena nasema, mkubalini Yeye aliye Amiri wa mambo yote.”—Mh.]

28 Bwana asifiwe! Sasa, simjui mama huyo, wala sijui ni nani aliyefasiri hayo, simjui mtu huyu, lakini sasa, kama mna shaka lolote kama ilikuwa ni kweli au la, ngojeni mpaka nitakapomaliza hadithi yangu.

29 Nilitaka Mungu ampige afe, akiangamize kitu hicho chote. Nikahisi hisia ya ajabu sana, nikarudi nyuma ya mlango. Sikilizeni, yale aliyosema, “Ni Mimi, Mungu, niliyetolewa.” Mnaona? Nami nikarudi nyuma ya mlango. Sasa, hili ni kwa ajili

yenu ninyi wanafunzi wa Kimethodisti humu jengoni, sikilizeni hili, naye Mungu ndiye Hakimu wangu, nikarudi nyuma ya mlango, nami nikasema. . .Kitu fulani kilikuwa kikiendelea, nami nikaangalia, na lilikuwa ni ono likisogea, ndipo nikaiona dunia, na kulikuwa na kitu kama du—duara ama ukungu mwekundu, ulioizunguka dunia, ukizunguka. Nami, ilionekana kana kwamba macho yangu yalielekezwa kwangu mwenyewe duniani, nikifanya mambo ya dhambi ambayo sikupaswa kutenda.

<sup>30</sup> Na kila wakati nilipoanza kufanya jambo baya, niliona lingepaa juu mbele za Mungu, na kama isingalikuwa ni kwa ajili ya Damu hiyo iliyofanya ukungu, ningalikuwa. Lakini Damu ya Yesu inatenda kama bamba kwenye gari, na kila wakati dhambi yangu ingemgusa Mungu, mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, ilionekana kana kwamba ingemgusa Yesu kabla haijafikia kile kiti cha enzi. Naye angekitikisa kichwa Chake, na machozi yangetiririka mashavuni Mwake, Naye angesema, “Baba, msamehe, hajui atendalo.”

<sup>31</sup> Ndipo ningefanya jambo lingine baya, ndipo basi ikaonekana kana kwamba Yeye alikuwa tu akitenda kama bamba kati yangu na mauti, kwa sababu Mungu alikuwa tayari ametangaza kifo changu: siku niliyotenda dhambi, hiyo ndiyo siku niliyokufa. Halafu basi, nisingeweza kuelewa, ni kwa nini ukungu huo umeizunguka dunia.

<sup>32</sup> Nami nikaangalia kule juu, ndipo basi kitabu cha—changu kikafunguliwa. Na hilo ni ono, kama tu ninavyoona humu jengoni, ila haya ni yale tu ninyi mmeyasababisha, hilo lilikuwa ni lile Mungu alitoa. Nami nikaona ya kwamba jina langu lilikuwa kwenye kitabu, na dhambi za kila namna ziliandikwa dhidi yangu kwenye kitabu hicho.

<sup>33</sup> Ndipo nikasema, “Bwana, je, dhambi zangu zilikufanya uteseke hivyo?” Naye alikuwa akilia, machozi yalikuwa usoni Mwake, na—na Yeye alionekana mchovu sana, maskini macho Yake yaliyoinama, vile niliona dhambi zangu zilikuwa zimemfanya ateseke. Nikasema, “Bwana Yesu, samahani. Ninasikitika kwamba dhambi zangu zilikufanya u—upate kuteseka kwa ajili yangu. Utanisamehe? Ninaahidi ya kwamba ni—nitakuwa mwema, nami nitafanya yote niwezayo, iwapo tu utanisamehe.”

<sup>34</sup> Ndipo akaugusa ubavu Wake kwa mkono Wake, kisha akaandika kutoka upande mmoja hadi mwingine wa kitabu hicho, “Amesamehewa,” akakisukuma nyuma ya mgongo Wake katika Bahari ya Usahaulifu, zisikumbukwe tena dhidi yangu. Ndipo nikapiga magoti, nikasema, “Ee Bwana, kamwe siwezi kuishi muda mrefu kutosha kukuonyesha shukrani zangu kwa Wewe kunisamehe dhambi zangu.”

<sup>35</sup> Akasema, “Sasa, nimekusamehe bure kila kitu ulichofanya, nawe unataka kumwangamiza.”

<sup>36</sup> Hilo lilinifunza somo. Wakati hilo ono liliponiacha... Sasa, angalieni tafsiri hiyo, “Mungu alitolewa kwa ajili yetu.” Mnaliona? Kikamilifu kwa maneno ambayo... Kabla sijalisema... Na kuna watu walioketi hapa kutoka kanisani mwangu, na kadhalika, ambao wamenisikia nikisimulia hadithi hiyo hapo awali, na kujua ya kwamba hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Mnaona? Inaonyesha jinsi Roho huyo wa Mungu alivyo mkamilifu, akinena pale katika lugha zisizojulikana, na kuzifasiri, pasipo mmoja wao kunijua mimi, wala chochote kile... .

<sup>37</sup> [Dada mmoja ananena kwa lugha, ndugu fulani anafasiri, “Naam, hivi ningemfanya nabii Wangu alie? Naam, ningemtuma akatafute, isipokuwa ilikuwa ni kwa ajili yako? Naam, nawaambia, usiku wa leo, enyi watu wangu, ni Mimi, Mungu, ninayesimama mbele yenu. Naam, hivi hamtanifuata? Naam, si Mimi Ndi—Ndiye niliyewapenda? Naam, si mimi Ndiye niliyebeba maovu yenu? Naam, si mimi Ndiye niliyeteseka? Naam, mtaniacha nilie? Naam, mtaniacha niwalilie? Naam, nawaambieni, usiku wa leo, msiogope, kwa kuwa nimesimama, naam, nimesimama tayari kupokea. Mtakuja? Asema Bwana.”—Mh.]

<sup>38</sup> Bwana asifiwe! Sikilizeni hilo. Hebu kidogo. “Mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini?”

<sup>39</sup> Mnajua nilichofanya? Sasa, angalieni hii hadithi inapoendelea. Nilimwendea mwanamke huyo, nikisimama huko nje. Nikasema, “Baba, nisamehe.” Nikamwendea, nikasema, “Naweza kuketi chini?”

Akasema, “Loo, halo.” Akasema, “Ni—nina mwenzangu.”

<sup>40</sup> Nikasema, “Mama, sikumaanisha hivyo.” Nikasema, “Ningetaka tu kuketi hapa kwa muda kidogo tu, mpaka marafiki zako watakaporudi.” Niliona alikuwa anakunywa pombe.

<sup>41</sup> Naye akasema, “Sawa kabisa.” Nami nikamsimulia hadithi niliyosimuliwa na lile ono. Akasema, “Ninajua wewe ni nani,” akasema, “Wewe ni Bw. Branham aliye hapa chini kwenye lile jengo la ghala la silaha.”

Nikasema, “Naam, mama, mimi ndiye.”

<sup>42</sup> Akasema, “Nilipitia kwenye mkutano wako hivi majuzi usiku, nisingeweza kuingia.” Akasema, “Bw. Branham, nimepita matumaini.” Akasema, “Baba yangu alikuwa mhubiri wa Kimethodisti, nina binti wawili ambao ni walimu wa shule ya Jumapili ya Kimethodisti.”

Nikasema, “Ilikuwaje?”

Akanisimulia hiyo hadithi. Akasema, “Hakuna tumaini kwangu.”

<sup>43</sup> Nikasema, “Mama, kama hakuna tumaini kwako, basi kwa nini Mungu akanionyesha ono hilo?” Na hapo huku tumeshikana mikono, nikamwongoza moja kwa moja katikati ya hiyo sakafu, kisha tukapiga magoti pale, tukawa na mkutano wa maombi, na kumrudisha kwa Mungu, pale pale.

<sup>44</sup> Huenda kukawa na mtu hapa ndani, usiku wa leo, katika hali hiyo. Neema ya Mungu, imemiminiwa mioyoni mwetu na Roho Mtakatifu. Mnaona?

<sup>45</sup> Ninaukumbuka mkutano huo vizuri, mwanangu. Inanikumbusha jambo hili: Haidhuru huyo mtu amefanya nini, wapendeni, na hilo ndilo linalowashinda.

<sup>46</sup> Kesho alasiri, sasa, msisahau hizo ibada, Bwana akipenda, tunataka kuwaombea wagonjwa.

<sup>47</sup> Nami ninataka kutoa tamshi hili kabla sijachukua somo langu, kwamba, jana jioni, wakati upako wa Roho Mtakatifu. . . Ambapo sikutaka, kwa vyovyote vile, kuwa na ibada ya namna yoyote kama hiyo, ilikuwa imetoka akilini mwangu kabisa, nilikuwa ninaenda kuwachukua ndugu zangu na kushuka miongoni mwa watu hao waliokuwa wameketi hapa katika vitanda vya wagonjwa, machela, wakifa, viti vya magurudumu, na kadhalika, na kusimama pale chini, na kushikilia. . . Nami nikamwambia Ndugu Hearn, ya kwamba nilipowatuma ndugu zangu hapa chini, ili asimame karibu nami, niliwataka waninii. . . Nilijisikia tu baada ya kuomba, na kula kwa nadra juma zima, kuninii. . . kwamba jambo fulani lingetukia hapa ambalo lingewafanya watu waamke.

<sup>48</sup> Ila tu, Mungu anaweza tu kufanya kazi palipo na imani. Nami nikawazia yale mahubiri magumu, na kadhalika, hakika yangewafikisha watu mahali fulani, na thibitisho la Uwepo wa Roho Mtakatifu lingekuwa kamilifu sana, hata wasingeweza kutilia shaka. Na katika kufanya hivyo, ni—niliketi, namna hiyo, nikiamini kwa moyo wangu wote ya kwamba Mungu angefanya jambo fulani kwa njia hiyo. Ndipo muda si muda mwajua, upako ukashuka, ulianzia huko nje kwenye jengo lile, ukiwashika wale watu waliokuwa wakifa huko nje, katika hiyo hali, nao huu hapa unakuja, moja kwa moja kwenye mstari huo, ukiwaponya watu hao moja kwa moja kupitia hivyo vitanda vya wagonjwa na machela, ukivifagilia mbali vitu hivyo vyote wakati ukipita.

<sup>49</sup> La mwisho ninalokumbuka nilikuwa mahali fulani pale, huku watu wakiinuka kutoka kwenye viti vyao vya magurudumu, na vitanda vya wagonjwa, na machela, na kuponywa, hilo lilikuwa karibu jambo la mwisho nililokumbuka. Kulikuwa ni kumwagwa kutukufu sana kwa Roho Mtakatifu.



<sup>50</sup> Sijui kama mtu yeyote angeweza kuketi chini ya upako wa aina hiyo, kisha ageuke, aseme, “La, si—si—sininii. . .” Ninaamini ya kwamba kwa namna fulani ingekuwa ni vigumu kwako kuponywa kamwe, kama—kama usingeweza—kama usingeweza kuupokea chini ya huo, si—sidhani kungekuwa na njia yoyote ya wewe kuingia tena, mnaona, chini ya upako kama huo. Sasa, huo ulikuwa ni wakati wa ajabu sana!

<sup>51</sup> Sasa, kusema kweli, tangu nilipoondoka, sikuzote nimekuwa katika miamsho tangu Desemba. Na sasa, nimekuwa mahali ambapo watu wamejaa sana, na mikutano mikubwa zaidi na kadhalika, bali sikujua wakati wowote ambapo Roho Mtakatifu aliwahi kutia mafuta kwa upako kama huo kwa ajili ya uponyaji, kama ilivyokuwa papa hapa jana usiku. Hiyo ni kweli. Nami ninashukuru sana kwa ajili yake.

<sup>52</sup> Nanyi kumbukeni tu, ya kwamba kuna watu waliokuwa hapa jana jioni, ambao mtasikia kutoka kwao, wame—wameponywa, wala hawajui. Mnaona? Wa—wao wanatarajia tu kwamba huenda jambo fulani likawapata wote mara moja, si lazima litokee hivyo, mradi tu kuna *kitu fulani* mle ndani kinachosema, “Naam, hilo latosha,” sijali inachukua muda gani. Kwa hiyo, ninyi wahudumu kumbukeni ya kwamba makanisani mweni mtakuwa mkiwaona watu wakija, wakisema, “Vema, mwajua, si—sina huo tena.” Mnaona?

<sup>53</sup> Halafu basi, mwanangu alikuwa akiniambia ya kwamba huyo mama alipitia hapa, huenda yuko hapa sasa, akisema, “Angalia macho ya mtoto wangu, hebu toa miwani,” mwenye makengeza ya kutisha sana, akatoa miwani, naye Billy akasema hayo macho yalikuwa yamenyoka kuliko yake. Kwa hiyo, kuna ninii tu. . . Ni ninii tu, hivyo ndivyo ilivyo. Mnaona, hakuna mtu aliyeyagusa. Mnaona, hilo ndilo ninalojaribu kuwaambia watu, ni kwamba sio kama tutakugusa au la, ni wewe kungusa *Yeye*. Mnaona? Imani yako ndiyo inayokuponya.

Sasa, usiku wa leo, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu, tunapofungua kurasa za hiki Kitabu. Halafu basi, kwa hiyo, tutulie.

<sup>54</sup> Bwana Yezu, tunakaribia kiti Chako cha rehema tena, na kuomba mwongozo wa Kiungu, usiku wa leo, upate kutuelekeza katika mawazo yetu, na ninii yetu. . . Tukijua, usiku wa leo, ya kwamba mioyo yetu ina furaha zaidi, kama Daudi alivyosema, wa kale, “Kikombe changu kinafurika.”

<sup>55</sup> Na jinsi ambavyo tunajua, baada ya mkutano kama huo jana usiku, ilionekana kana kwamba, Bwana, ya kwamba mji huu wote ungewashwa moto! Lakini wako wapi? Bwana, kweli, tungewezaje ila kuamini kwamba Wewe uliwachagulia Uzima, ama, kwa kujua Kwako tangu zamani, Wewe ulijua ni nani angekupokea Wewe, na ni nani asingekupokea! Mtu anawezaje kuja, ambapo Mungu hajamwita, wala hajamchagulia uzima?

Kwa hiyo tunatambua kama vile imekuwa kote katika nyakati, ndivyo ilivyo sasa, kwamba maskini wanadamu wenye mashaka, waliopofushwa, hata hivyo watu wengi wenye moyo mkarimu, watu wazuri, wanaoishi maisha mazuri, ya haki, kuhusu uadilifu, na hata hivyo wamepotea kabisa na wameisha, bila tumaini, bila Mungu, bila rehema, katika saa hii yenye giza, ya kufa.

<sup>56</sup> Baba, moyo wangu unatokwa na damu, na kusihi, wala sijui nifanye nini tena, lakini kuendelea tu kutoa sauti yangu, ili kwenye Siku hiyo, itakuwa kwenye kanda ya sumaku Utukufuni.

<sup>57</sup> Nami naomba ya kwamba utaendelea kuwa pamoja nasi na kutusaidia. Bariiki ibada za kesho, ndugu zangu wahudumu wanapohudumu makanisani mwao. Loo, jalia kuwe na Moto kutoka Mbinguni juu ya kila madhabahu! Tujalie, Bwana. Jalia kuwe na ibada kuu kote kwenye taifa na kote nchini kesho, na uwaokoe wote wanaoweza kuokoka.

<sup>58</sup> Zibariki ibada usiku wa leo, na Maneno haya machache, Bwana, ambayo yamesomwa alasiri ya leo, hapa katika Maandiko, na ambapo nimechagua kuzungunza maneno machache, usiku wa leo. Na iwe hivyo, kwamba wengi watapokea imani na kumwamini Yesu, kwa kuwa tunaomba, katika Jina Lake. Amina.

[Ndugu fulani ananena kwa lugha—Mh.]

<sup>59</sup> Um-hum. Roho Mtakatifu huenda . . . Kwa kawaida jumbe huja tatu-tatu; hakuwezi kuwa na zaidi ya jumbe tatu kwa wakati mmoja, kulingana na Maandiko. Lakini huo ndio ujumbe wa tatu, na huenda ikawa ni Roho Mtakatifu akijaribu kuufikishia mtu fulani, kwa hiyo iweni na kicho kabisa, kila mtu.

<sup>60</sup> [Ndugu fulani anafasiri, “Naam, wewe uliye na sikio la kusikia, na asikie yale Maandiko yasemayo. Nami niliwaambia wanafunzi Wangu, nilipowaenda wakienda zao Emau, ya kwamba kama wangeamini tu, na kwa kuwa mioyo yao ilikuwa imefunguliwa kwa Maandiko, nilipokuwa nikiwaambia maneno ya Uzima, mioyo yao iliwaka ndani yao, kama tu mngeyafungua macho yenu mpate kuona, masikio yenu yapate kusikia, mtaamini, nanyi mtapokea utukufu wa Mungu.”—Mh.]

Amina. Asante, Bwana.

Ningetoa kutoka kwa hilo, kwamba wangekuwa kama . . . kwamba Yesu . . . Haya hapa maombi yangu Kwake, juu ya jumbe hizo:

<sup>61</sup> Mungu, jalia iwe, usiku wa leo, wakati . . . Tufungie ndani kama ulivyowafanya wale waliotoka Emau, na jalia tuone, usiku wa leo, Wewe ukifanya jambo fulani miongoni mwetu kama ulivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, ili walimwengu walio hapa, usiku wa leo, ama, Kanisa, wapate kujua ya kwamba umefufuka katika wafu.

62 Jalia Yeye . . . Walijuaaje Yeye alikuwa ni Yesu yeye yule? Kwa sababu alifanya mambo yale yale aliyofanya.

63 Sasa, tafadhalini, kila mtu baki kitini mwako, na uwe na kicho kabisa, ninawaomba katika Jina la Yesu, ketini, mwe na kicho kabisa, na msikilize.

64 Sasa, Roho Mtakatifu amenena kupitia aina fulani ya karama, ya lugha na tafsiri, hakukuwa na jambo moja katika hayo ambalo nisingeliheshimu, bali kuamini linatoka kwa Mungu. Na sasa, limekuja kabla sijasoma Maandiko, halipaswi kutolewa tunapohubiri, “Roho wa manabii humtii nabii.” Na sasa, limekuja kwa utaratibu, vema. Na, sasa, inaonekana kana kwamba Yeye anajaribu kusisitiza kwamba Mungu atafanya jambo fulani, hata hivyo, sijagawa kadi zozote za maombi kwa ajili ya ibada ya uponyaji, lakini jambo fulani huenda likatukia, sijui.

65 Lakini mliona ilikuwa ni nini? Huyu Yesu, wakati Yeye . . . Walidhani alikuwa amesulubiwa, na alikuwa amekwisha, bali alizungumza nao siku nzima, wasimtambue. Ndipo basi usiku huo, aliwaingiza chumbani na kufunga mlango, alipokuwa katika nyumba ya wageni, ndipo akafanya jambo fulani, kama tu alivyofanya, hakuna mwingine aliyelifanya namna hiyo, Naye alilifanya jinsi tu alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, nao . . . Ndipo basi akafanya nini? Akakatoweka gizani. Nao wakakimbia huko nyuma kabisa kwa watu wao, na kusema ya kwamba kweli Yesu alikuwa amefufuka katika wafu. Walijua hilo, kwa kuwa walijua Yeye alifanya jambo fulani kama tu alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, ilikuwa ni thibitisho ya kwamba ilikuwa ni Yesu yeye yule, aliyefufuka katika wafu. Na afanye jambo lile lile.

66 Na tutakapoondoka hapa, usiku wa leo, tukienda kwenye makazi yetu mbalimbali, jalia tuweze kusema kama wale waliotoka Emau, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?”

67 Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 14, kifungu cha 8:

*Maana baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejifanya tayari kwa vita?*

68 Nami ninataka kuzungumza juu ya somo la *Sauti Isiyojulikana*. Sasa, Paulo alikuwa akizungumza (Hilo si ni ajabu?) juu ya jambo lile lile hapa, kuhusu kutoa lugha na kufasiri. *Sauti Isiyojulikana*.

69 Sasa, tunaishi katika siku ya kutokuwa na hakika. Tunaishi katika siku ambapo karibu kuna kila kitu, karibu kila kitu, ambacho tunaweza kuweka mikono yetu juu yake, cha kawaida, hakina uhakika. Kuna mashaka mengi sana hata mataifa yana—yanatetemeka. Kuna mashaka katika usalama wa taifa letu; hakuna taifa lililo salama tena.

<sup>70</sup> Ama tungeweza kuwa ma—mateka wa Urusi, kufikia usiku wa manane leo hii, au ama tulipuliwe vipande-vipande, inategemea kile Urusi inataka kufanya juu yake.

<sup>71</sup> Tunazungumza juu ya wanasayansi wetu, wanao watu ambao wanaweza kuwaweka maili mia mbili hewani, katika mtambo mdogo utakaokuja huku moja kwa moja, wawaweke moja kwa moja juu ya taifa hili, na kutuma ujumbe huku chini, na kusema, “Ama mjisalimisha, la sivyo tuvute wenzo, na ni hayo tu.” Sio lazima wangoje hadi kesho kufanya hivyo, wanaweza kufanya hivyo sasa hivi.

<sup>72</sup> Kama tuna akili timamu, tungefanya nini? Je, Pe—Pentagon ingefanya nini, ta—ta—taifa lingefanya nini? Lingejisalimisha, ingewabidi kujisalimisha. Ndipo ingekuwaje? Wimbi baada ya wimbi la askari wa Urusi wangepanda waingie humu nchini mwetu, wakiwabaka wanawake wetu, wakichukua nyumba zenu, na kuwafukuza mtaani, na kuwapiga risasi, na kuwaua watoto wenu mbele yenu, na kuliteka hili taifa. Ndipo tungejua kile dhambi...jinsi tumekuwa...ilichomaanisha kuichekelea ibada ya kidini, na kuwaita kundi la watakatifu wanaojifingirisha, ama...Kumbukeni, linakuja. Hakuna usalama wa taifa.

<sup>73</sup> Tu—tuko—tuko kwenye—tuko—tuko kwenye—tuko, kwenye ile karamu ya Belshaza, tena. Walidhani kwa sababu walikuwa ndani ya kuta hizo kubwa, wanasayansi wa—walio bora sana, magari yaliyo bora sana (Wangeweza kuendesha magari matatu au manne sambamba kuuzunguka ukuta huo wa Babeli na—na pasipo kusogeza ninii...kupoteza farasi, ama gari. Na yale malango makubwa mno, ambayo labda yalikuwa nusu...loo, upana wa futi arobaini, hamsini, namna hiyo.), hapakuwapo na taifa lingeweza kuwafikia, ama chochote kile, kwa hiyo waliishi tu katika dhambi, vyovyote walivyotaka. Lakini Mungu anaweza kuangalia juu ya ukuta.

<sup>74</sup> Nao walikuwa na ka—karamu kubwa ya kawaida ya chai usiku mmoja, ama shamrashamra kubwa za ulevi, ndivyo ilivyokuwa, kitu kama baadhi ya vipindi vyetu vya kisasa vya televisheni, ambapo wao, baada ya kulewa kwelikweli, walidhani wangeweza kufanya mizaha michache kuhusu yule mhubiri mwenye upara, ama kitu kama hicho. Basi ilikuwaje? Walienda na kuvichukua vyombo vya Bwana, na kuvinywea divai kufanya dhihaka. Basi usiku huo, huo ulikuwa, mnakumbuka, huo ulikuwa ndio mwanzo wa ufalme wa Mataifa.

<sup>75</sup> Ninataka kuwaulizeni ninyi watu jambo fulani ambalo kidogo huenda ikawa ni muhimu. Mtu yeyote anayejua Biblia, anajua ya kwamba Mungu alianza...alishughulika na Wayahudi mpaka Mfalme Nebkadreza; kile kichwa cha dhahabu kilikuwa ndio mwanzo wa milki ya Mataifa, inaishia kwenye miguu huko Rumi. Hiyo ni kweli, ndugu, enyi wanafunzi

wa Biblia? Angalieni kinachotukia. Ilifanya nini mwishoni mwa ufalme huo? Kulitokea maandiko ya mkono kwenye ukuta yaliyokuwa katika lugha zisizojulikana. Hakuna mtu angaliweza kuifasiri, bali walikuwa na mtu pale aliyekuwa na karama ya kufasiri. Kwa hiyo, akaja na kuyasoma hayo maandiko ya mkono kwenye ukuta.

<sup>76</sup> Nayo yamesomwa hapa tena, usiku wa leo, na Roho wa namna ile ile, yakitolewa na Mungu yeye yule. Maandiko ya mkono yako kwenye ukuta, wakati wote ambao tumekuwa tukitumia pesa zetu, na mizaha, na kadhalika, tunakuwa tu kundi kubwa la wacheshi, tukiicheka dini, tukiidhihaki, na wakati wote Urusi imekuwa ikiweka vitu hewani ambapo wametushinda kwa mbali sana, mpaka wako miaka na miaka na miaka mbele yetu. Mnakumbuka Wamedi na Waajemi walikuwa langoni, wakingojea, wakati mambo haya yalipotukia, nao hawakujua chochote juu yake.

<sup>77</sup> Hakuna tena usalama wa taifa. Wanapowaambia tuko salama, kwamba tunaweza kufanya *hivi* ama kufanya *vile*, wamekosea. “Chimbeni shimo ardhini,” baadhi ya upuuzi huu hapa wa usalama wa taifa, “mkakimbilie ardhini,” huku bomu hilo litalipua shimo ardhini lenye kina cha futi mia moja na hamsini, mia moja na . . . maili mraba, vema, kama ungekuwa futi elfu tano chini ya ardhi, ungekuwa kwenye lava, na kama ungekuwa futi elfu tano chini ya ardhi, huo mtetemo ungevunja kila mfupa mwilini mwako.

<sup>78</sup> Kwa hiyo huwezi kuchimba chini upate kulikwepa, hakuna njia hata kidogo ya kulikwepa. Kuna—kuna kimbilio moja tu unaloweza kuingia chini yake, wala kimbilio hilo halijatengenezwa kwa chuma, limetengenezwa kwa manyoya, chini ya mbawa Zake. Haleluya, Yeye ana nguvu; hilo ndilo kimbilio la pekee. Panda juu yake. Kunyakuliwa, kunakuja.

<sup>79</sup> Sasa, kuna amani ya mahangaiko. Haikubidi uwazie, mataifa makubwa mno kama Urusi, mataifa madogo sana yanaweza kufanya hivyo. Tuko tu kwenye mwisho wa safari.

<sup>80</sup> Na jamani, wanafanya nini? Moja . . . Tunauza vitu vingi sana kwa taifa moja, tukijaribu kununua urafiki kwa pesa zetu, na Mhindi mwenyewe ambaye tumemnyang’anya hizo pesa, au, kumnyang’anya ardhi, tunamwua kwa njaa huko nje mbugani, na kumnyang’anya kondoo, na kumwacha aishi huko nje na TB, na kadhalika, katika hema, halafu tunatuma pesa ng’ambo, huko, tukiuita *ulinzi wa taifa*, tukijaribu kununua urafiki. Huwezi kununua urafiki. Tunatumia mamilioni ya dola kila mwaka kwa wiski na bia, huku wamishenari wetu hudumani, wakifa kwa njaa. Ni kweli.

<sup>81</sup> Loo, hakika, tumekwisha, hili taifa limekwisha. Mataifa yote yamekwisha, si taifa hili pekee. Nafikiri hili ndilo malkia wa mataifa, ni kweli, ndilo ustaarabu mkuu, wa mwisho tulio

nao, lakini limekwisha, yote yamekwisha. Tuko tu tayari kwa ajili ya Kuja kwa Bwana. Hiyo ni kweli. Kanisa likijiweka Mwenyewe tayari. Ifikapo wakati nitakapomaliza, kesho alasiri, Bwana akipenda, mtaona kama si kweli. Sasa, kwa—kwa Neno la Bwana, mwone kama hiyo si kweli.

<sup>82</sup> Sasa, kumbukeni ya kwamba hatuwezi kuweka matumaini katika mahali popote pa usalama wa mataifa, tena. Tukienda Urusi, ni . . . iwe kwamba tutawalipua; kama wakisema *hapa*, wao watatulipua; kama tukienda Japani, itakuwa ni jambo lile lile tu; liko tayari kuvunjika vipandevipande sasa hivi. Wala hakuna vile unayoweza kulikomesha, kwa sababu wamepuuza kufanya yale hase Mungu aliyowaambia wafanye, na badala ya kuihubiri Injili, wamejenga majengo, na walikuwa na utaalamu mzuri, na elimu, wametumia wazo lao wenyewe kuwaelimishia watu.

<sup>83</sup> Naye mtu huyu aliye mahakamani, Mjerumani huyu sasa, mwerevu, mwenye akili, jitu la kielimu, kisha mchukueni huyu Eichmann, aliyewagandisha hao watu hata wakafa, kisha akawatupia maji moto, na kuwaua hao mamilioni, na nilipokuwa Ujerumani, huko katika sehemu zile ambamo waliwapeleka huko nje na kuwadunga mapovu hayo kwenye mishipa yao, Hitler, na kuwatuma huko nje, na wanasayansi werevu, wenye elimu, ya juu zaidi (Mbona, tulikuwa . . . nusu ya vita ilikuwa imekwisha kabla hatujapata kuwa na bunduki ambayo ingeweza kulinganishwa na .88 yao. Vipi kuhusu ninyi askari mliokabilia nayo? Mnajua hiyo ni kweli. Mbona, sisi . . .), wametupita kwa mbali katika sayansi, na werevu, na kadhalika namna hiyo, nao wangegeuka na kufanya jambo kama hilo? Ni wendawazimu.

<sup>84</sup> Na vijana wowote wanaoweza kusimama katika jengo huku wameinua mikono yao juu kwenye makelele haya yote ya roki, na kadhalika, na uhuni, ni wendawazimu! Ni hatari. Wamekwisha, zile nguvu za akili zimeharibika. Kumbukeni, ule mti wa maarifa hufikia tu *umbali huu* kisha unarudi kinyumenyume.

<sup>85</sup> Kwa hiyo hapo ha—hatuna sauti ya usalama katika usalama wa taifa. Kazi zetu, hatuna usalama katika kazi ze—zetu, zote hazina uhakika. Hebu mtu apite umri wa yapata miaka thelathini na mitano, watakung'oa, watamchukua kijana ili isiwabidi kukustaafisha. Na baada ya kupita umri wa miaka arobaini, ukijaribu kutafuta kazi, hata ya kuchimba mitaro, itakubidi kuwa na diploma ya shule ya upili kabla hujaweza kuifanya. Wana kitufe kidogo wanachoweza kubonyeza, nacho kinashughulikia hizo kwa vyovyote vile. Kazi zenu, hamna usalama wowote katika kazi zenu.

<sup>86</sup> Sijui jinsi hili lilivyo kweli, lakini nimeambiwa ya kwamba kuna watu wengi zaidi wasio na kazi sasa hivi, kuliko ilivyokuwa wakati wa kuzorota kwa uchumi kwa Rais Hoover, kwa sababu

kuna watu wengi zaidi. Kuna shida gani? Ni mahali tu ambapo hakuna uhakika katika mambo haya. Huna hakika na kazi yako, mtu fulani anaweza kuchukua mahali pako asubuhi.

<sup>87</sup> Siasa... Hebu tuzungumze tu kidogo, usiku wa leo, hii ni Jumamosi usiku. Siasa, ati ni potovu? Pande zote mbili, zimepotoka sana ziwezavyo kuwa. Iithibitika katika uchaguzi huu uliopita, wakati FBI ilipolifichua jambo hilo, ya kwamba walikuwa na mitambo ambayo kila wakati walipompigia kura mtu mmoja, Bw. Nixon, iliwabidi kumpigia kura Kennedy wakati uo huo, nao wakalithibitisha. Nao walifanya nini juu yake? Hakuna kitu. Sasa, mimi si Mwanademokrati, wala Mripablikani, si hata mojawapo, mimi ni Mkristo. Kwa hiyo mtu, chungu hakiwezi kusema birika ni jeusi, ama limejaa grisi, moja ni jeusi tu kama jingine, chafu tu kama jingine.

<sup>88</sup> Lakini kuna shida gani? Ni kwa sababu kwamba hakuna usalama katika mambo hayo, yamekwisha. Bunge kuu la Wananchi Uingereza, wakati mmoja lilisema, kuhusu demokrasia, lilisema, "Demokrasia ni chombo baharini kisicho na nanga." Kasema, "Itakuwa kwamba wanasiasa watasimama juu ya masanduku ya sabuni, na kufanya uchaguzi Marekani, na kutoa hongo wapate kuingia..." Hiyo ni kweli kabisa, bali hakuwazia kuhusu Bunge lake zuri, la kupendeza la Mabwana lingefanya vile vile. Kwa hiyo inaonyesha ya kwamba vitu hivi vyote vimeoza na kuharibika, kwa sababu unakuja Ufalme ambao Mwanzilishi wake, Mji ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu. Mambo haya hayana budi kusambaratika.

<sup>89</sup> Siasa yote ni... Ninaamini demokrasia, bila shaka, mimi ni Mmarekani, nami ninaamini demokrasia, lakini, loo, jamani, kwenye mambo yaliyoza yaliyo katika demokrasia! Jambo ndilo hilo. Kwa hiyo, inaonyesha ya kwamba mawazo haya yote ya kujibunia ya kidunia hayana budi kuuondokea Ufalme ujao.

<sup>90</sup> Nimekuwa na majaliwa ya kusimama kwenye yale maeneo huko Misri, ambapo mafarao walisimama na kuwaua watu, ambapo wapiganaji wa kutumbuiza, na kadhalika, unachimba futi ishirini chini ya ardhi upate ufalme wao, mahali ulipokalia. Nimesimama mahali mafarao waliposimama, nimekaa mahali ambapo ninii... na ya—yale majumba makubwa ya michezo, na—na mahali mbalimbali huko—huko Rumi, na ninii... na katika... mafarao, na kadhalika, nazo falme zao zimeanguka, na badala ya kuangalia tu hapa nje kuziona, inakubidi kuchimba chini upate kuona magofu yao. Kuonyesha ya kwamba kila ufalme wa kujibunia, kila mfumo wa kujibunia, hauna budi kutoweka.

<sup>91</sup> Kwa hiyo, mnaona, sijali ni demokrasia ya namna gani, tunajenga UN ngapi, ni Mashirikisho mangapi ya Mataifa, ama chochote tulicho nacho, yote yanaoza.

Wakati umejaa badiliko la haraka,

Hakuna kitu thabiti duniani  
kitakachosimama,  
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,  
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Safari hii itakapokamilika,  
Na kwa Mungu umekuwa mkweli,  
Nyumba yako nzuri na angavu Utukufuni,  
Nafsi yako iliyonyakuliwa itaona!

<sup>92</sup> Sijali unaweza kupata pesa ngapi, ama ni majengo mangapi ungeweza kujenga, ama ungekuwa rais mara ngapi wa kampuni yoyote, inaanguka, inaporomoka.

<sup>93</sup> Wazo liko moyoni mwangu sasa, juu ya ujumbe wa yule malaika wa tatu uliotolewa, Martin Luther, John Wesley, na malaika anayefuata. Ujumbe wa malaika wa mwisho ulisema nini alipovuka, wale malaika watatu? “Babeli imeanguka, imeanguka, imekuwa maskani ya kila roho chafu.” Hapo ndipo ilipo hasa.

<sup>94</sup> Hakika, hatuna usalama katika taifa letu. Halina uhakika kila mahali. Mashaka, kutokuwa na uhakika katika kazi yako, kutokuwa na uhakika katika siasa, kutokuwa na uhakika katika chama cha Democrat, kutokuwa na hakika katika chama cha—cha Ripablikani, kutokuwa na uhakika katika vyama vyote.

<sup>95</sup> Na kanisani, pia hakuna uhakika. Tunawezaje kuwa na yapata madhehebu mia tisa mbalimbali, na kila moja likitofautiana na lingine, na kisha kugombana moja na lingine? Maskini mlei anawezaje kujua la kufanya? Watu wanawezaje kujua mahali pa kusimama? Moja linasema, “*Tunayo* hapa,” lingine linasema, “*Tunayo* hapa,” na “*Tunayo* hapa chini.” Watu wanajuaje la kufanya? Ni kutokuwa na uhakika, kanisa linatoa sauti isiyojulikana.

<sup>96</sup> Siasa inatoa sauti isiyojulikana, taifa linatoa sauti isiyojulikana, ajira inatoa sauti isiyojulikana. Loo, ningeweza kuzungumza juu ya mambo mia moja ambayo hayana uhakika, hayana uhakika.

Kanisa la Kimethodisti linasema, “*Tunayo*.”

Kanisa la Kibaptisti linasema, “Unadanganya, *tunayo*.”

Mpresbiteri anasema, “Ninyi nyote wawili mnasema uongo, *tunayo*.”

<sup>97</sup> Wapentekoste wanasema, “*Tunayo*.” Angalia tu jinsi tunavyotengana, na kuzozana, na kugombana, na kila kitu, inaonyesha hatuna *hiyo*. Kweli kabisa. Kwa hiyo, hiyo ni sauti isiyojulikana.

<sup>98</sup> Sauti isiyojulikana, huwezi. . . Unasema, “Vema, tutaingia shimoni, na kuchimba ardhini, kwa ajili ya usalama wa taifa.” Jaribu wakati mmoja, uone kitakachotukia.



“Nina kazi, ndugu, nina ahadi.” Hebu tu wabadilishe mabosi wakati mmoja.

<sup>99</sup> Maisha ya nyumbani hayana uhakika. Mtu anaweza kuoa maskini mwanamke mzuri, amtoe barani, hapa, ambako hajaharibika, ampeleke nyumbani na kuweka televisheni humo ndani, na muda si muda wajua, unarudi nyumbani, yeye anatenda kama baadhi ya hawa mabingwa wa sinema.

<sup>100</sup> Kutokuwa na uhakika katika maisha ya nyumbani. Anawaacha watoto wake kuranda-randa mitaani huku wana nyuso chafu, na huko nje mtaani wakicheza, na kushika mkononi mwake maskini mbwa mdogo, mwenye pua koromaji, na kumpa upendo wa mtoto. Anambeba maskini mbwa mzee kwenye gari, huku anapanga uzazi. Aibu kwa wanawake Wamarekani! Ni jambo baya sana kusema hivyo. Sijui, lakini huu ni wakati mmoja mtakaolisikia, kwa vyovyote vile, kama mtatulia tu, wala msindelee kutoka nje. Mtu anaweza kushikilia *kiasi fulani* tu, halafu inawabidi kulipuka na kukimbia, lakini—lakini—lakini sikilizeni, hiyo ni kweli, ni kweli. Mtu fulani hana budi kukemea kitu hicho!

<sup>101</sup> Na kuna ndugu wengi wahubiri wazuri wanaosimama mimbarani wanaojua hiyo ni kweli. Lakini mimbara yao ni nini? Ni riziki kwao. Afadhali nilale kwa tumbo langu, na kunywa maji ya matawi, na kula biskuti za chumvi, nihubiri kweli, kuliko kula kuku wa kukaanga mara tatu kwa siku, na inilazimu kupatana juu ya Neno la Mungu. Sema kweli, maana huna budi kuwajibika kwake kwenye ile Siku ya Hukumu.

<sup>102</sup> Bila shaka, kuna mashaka, kutokuwa na uhakika. Loo, tunaona... Halafu mnasema, “Ndugu Branham, unatuweka kwenye tawi hapa nje.” Hiyo ni kweli, ili mpate kujua mahali mlipo.

<sup>103</sup> Mnasema, “Basi, Ndugu Branham, kuna kitu chochote kilicho na sauti dhahiri?” Naam, bwana. Kuna Kitu kimoja kilicho na sauti kamilifu, dhahiri. Ni kitu gani? Ni Neno la Mungu. Ni Sauti ya hakika, ni kamilifu, ni Sauti ya Milele.

“Una hakika na hilo?”

Yesu Kristo alisema katika Mathayo, mlango wa 24, kifungu cha 35, Yeye alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.”

Matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu kingine  
Ila Damu ya Yesu pamoja na haki;  
Wakati yote yanayoizunguka nafsi yangu yakitoweka,  
Basi Yeye ndiye tumaini langu lote na ngome yangu.

Kwa kuwa juu ya Kristo, ule Mwamba imara,  
 ninasimama;  
 Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao,  
 Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

<sup>104</sup> Sasa, Neno la Mungu, ahadi Zake, ni za kweli. Sasa, kuna jambo moja tu la kuendea chochote. Kama vile Israeli, Israeli walikuwa mfano mkamilifu wa taifa hili. Israeli walikuwa ni watu wanaomcha Mungu waliokuwa katika utumwa wa ninii. . . kwa Wamisri. Nao wakaiacha nchi hiyo ya utumwa, wakaanza safari. Sikilizeni sasa, msikose kupata hili. Mungu na afungue ufahamu wenu. Waliacha nchi yao ya *kusafiri*, wakaja kwenye nchi yao ya ahadi, na kuwasukuma nyuma wenyeji, kisha wakakaa katika hiyo nchi. Hiyo ni kweli?

<sup>105</sup> Tulifanya jambo lile lile. Tulikuwa chini ya Ukatoliki, na utumwa wa. . . nasi tulitaka kuwa watu wacha Mungu waliompenda Mungu, na waliokuwa na uhuru wa dini, ndipo tukaja kwenye taifa hili, tukawarudisha nyuma wenyeji, na kuimiliki nchi.

<sup>106</sup> Mradi tu. . . Wakati Israeli walipoanza kutoka, walikuwa na viongozi wacha Mungu, Daudi, Sulemani, walileta heshima. Mbona, Israeli ilijulikana kote ulimwenguni, kwa mataifa yote, nao wote waliwaheshimu. Hiyo ilionyesha kile Mungu angeweza kufanya na kundi la wanaume na wanawake waliomcha Yeye, na kuishi kitauwa mbele Zake.

<sup>107</sup> Kama nilivyohubiri siku chache zilizopita usiku, hata yule malkia wa kusini alikuja kote kupitia Jangwa la Sahara, miezi mitatu juu ya ngamia, kusikia hekima ya Sulemani. Ulimwengu mzima uliwatazamia.

<sup>108</sup> Na wakati taifa hili lilipoanzishwa, tulikuwa na watu wacha Mungu waliolianshiza, George Washington, Abraham Lincoln. Bonde la Forge, wakati, alipoomba usiku kucha, kiongozi huyo, ndipo risasi zikapitia kotini mwake kesho yake, bila kuko- . . . bila kumpiga! Abraham Lincoln, mtu mcha Mungu!

<sup>109</sup> Tulifanya nini siku chache zilizopita? Tulifanya jambo lile lile walilofanya Israeli, tukamchagua Ahabu kwe—kwenye Ikulu. Sasa, Ahabu alikuwa ni jamaa mzuri sana. Alitaka kutubu, lakini Yezebeli, alikuwa amemwoa, wala asingeweza kufanya hivyo, ndiye aliyekuwa shingo iliyokigeuza kichwa. Nasi tulifanya jambo lile lile, tukamweka mtu huko juu ambaye ameolewa na mfumo huo wa Yezebeli tulioukimbia, nasi tukawa taifa huru kwake. Loo, ninyi wanasiasa, mliouza haki zenu za mzaliwa wa kwanza za Ukristo! Nitakomea juu ya hilo. Hebu turudi nyuma. Mungu ameliahidi na Mungu alisema lingetukia, Ufunuo 13, kwa hiyo hakuna njia ya kulikwepa, ninawatakeni tu mjue mahali mnaposimama, yale mliyofanya.

<sup>110</sup> Na baadhi yenu watu wangu weusi wa thamani mliopiga kura namna hiyo, mbona, mmeleta fedheha kwa damu ya

Abraham Lincoln aliyetoa mkanda wa utumwa kutoka kwa baba zenu! Kweli kabisa. Nisingedhania mngefanya hivyo. Jamani, hivi hamjui mlilofanya? Kwa nini mkajiuza kwa do—dola chache za ziada, mungu wa tumbo badala ya Mungu wa moyoni? Hizo ndizo mataifa yameziendea, ni dola chache za ziada.

<sup>111</sup> Hiyo ndiyo shida ya Ahabu. Lakini, ndugu, walikuwa na maskini nabii mmoja kule chini ambaye hakupatana nao, aliwakemea. Kila moja ya hayo madhehebu lilimfukuza, walimchukia, bali hakika aliwaambia yaliyo kweli. Basi alipomaliza kumkemea maskini Yezebeli huyo aliyejipodoa, kuhusu hao wanawake, jinsi walivyokuwa wakitenda, wote walimchukia. Lakini siku moja Mungu alisema, “Umehubiri muda mrefu vya kutosha, ondoka uende huko nje nyikani, sasa nitatuma hukumu.” Nayo ikaja, Yeye akaituma.

<sup>112</sup> Loo, kwenye saa tunayoishi, enyi marafiki, bali kuna Kitu kimoja cha hakika, Kitu kimoja hakika, tunaona taifa letu limekwisha, tunaona ulimwengu umekwisha, kuna Kitu kimoja cha hakika Milele, na hicho ni Neno la Mungu, Kile Mungu alichosema, Mungu atalitimiza Neno Lake.

Hebu tuwachukue tu wahusika wachache ambao nimewaandika kwenye kipande cha karatasi hapa, ambapo ninapenda kuwarejea, wahusika wachache waliokuwa na hakika.

<sup>113</sup> Nawe unaweza kuwa na hakika. . . Huwezi kuwa na hakika ya Neno la Mungu kama ukilisoma tu, Mungu hana budi kunena na wewe kupitia kwa Neno.

<sup>114</sup> Sasa, Nuhu, Nuhu alikuwa na hakika kwamba itanyesha kadiri alivyoweza kuwa, alikuwa na hakika nalo. Hakukuwako na sauti isiyotambulikana wakati Mungu aliposema, “Nuhu, jenga nyumba, uh, safina ukajiandae kwa ajili ya wokovu wa nyumba yako.” Hiyo haikuwa sauti isiyojulikana. Ilionekana kana kwamba kwa watu haikuwa na hakika wakati mtu mshenzi, mkulima, alipopata wazo la kipumbavu kichwani mwake ya kwamba atajenga safina, wala hakujapata kunyesha, wala umande haukuwa umeanguka kutoka mbinguni, wala chochote kile.

Ninaweza kuwasikia wakosoaji wakisema, “Aisee, Bw. Nuhu, niambie, mvua inatoka wapi?”

Vema, huenda Nuhu alisema kitu kama hiki: “Nina hakika Hiyo ilikuwa ni Sauti ya Mwenyezi Mungu.”

“Vema, mvua inakujaje?”

<sup>115</sup> “Kama hiyo ilikuwa ni Sauti ya Mungu iliyosema inakuja, Mungu anaweza kuiweka juu kule ianguke chini.” Alikuwa na hakika itanyesha, kwa sababu Neno la Mungu lilisema hivyo, lilikuwa la hakika, naye alijua ilikuwa ni hakika.

<sup>116</sup> Nilipoanza kuzungumza asubuhi ya leo wakati nilipokatizwa na ikanibidi kuondoka, Musa, alikuwa mwanajeshi mkuu, tunaambiwa na wanahistoria, naye alijaribu moyoni mwake, akijua alikuwa ameitwa kwenye huduma. Sasa, ndugu, hili ni somo kwetu sote. Alijua alikuwa na wito katika huduma; tunajua hilo sisi wenyewe, bali hebu na tuangalie kile tunachofanya nayo.

<sup>117</sup> Musa alijua, mama yake alikuwa amemfundisha, kwamba alikuwa awe ndiye mkombozi. Alizaliwa mtoto mzuri, na jinsi alivyolelewa na mama yake, na kulelewa moja kwa moja chini ya mlango wa Farao, na kweli alikuwa na mguu wake kwenye kiti cha enzi. Alijua ya kwamba alikuwa awe mkombozi wa Mungu, bali alijaribu kufanya hivyo katika mfumo wake mwenyewe.

<sup>118</sup> Nasi tunajua sisi ni wahudumu, ambao Mungu alituita, lakini hebu tusijaribu kufanya hivyo kwa kuona tunawaingiza wangapi katika madhehebu yetu, tukifanya hivyo, tutafanya kosa lile lile walilofanya. Hebu tumfuate Roho, hebu twende pamoja na Mungu.

<sup>119</sup> Musa alikuwa, labda, kamwe hajaisikia Sauti ya Mungu, bali alijua kwa akili, alijua kwa hisia iliyokuwa ndani yake, ya kwamba alikuwa ndiye mkombozi, bali alijaribu kufanya hivyo akashindwa, kwa hiyo akasema, “Labda nilifanya kosa.”

<sup>120</sup> Huenda kukawa na wahubiri wanaoketi hapa nje vile vile, waliodhani mlifanya kosa, mlipoona kushindwa kwenu, kamwe hamkungeja muda mrefu vya kutosha. Biblia ilisema, “Wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya, watapaa juu kwa mbawa kama tai.”

<sup>121</sup> Musa alifikiri kwamba labda alikuwa ameukosa wito wake, lakini siku moja wakati Mungu aliponena naye uso kwa uso, naye akasikia Neno la Mungu, Malaika wangu akanena naye, nayo yakapatana na Neno, alipoona ya kwamba ile Sauti iliyonena naye ilikuwa ni kitu kile kile Neno lilichokuwa limeahidi, basi akawa na imani, naye akawa na hakika kwamba atashuka kwenda kule. Alikuwa na hakika Israeli itatoka chini ya utumwa, kwa sababu Mungu alifanya ahadi, ilikuwa ni ahadi ya Kimaandiko. Ndipo Sauti ikanena na Musa, na kusema, “Nimesikia kilio cha watu wangu, nami nimekumbuka agano langu kwa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, nami ninakutuma huko chini huko ukawakomboe.”

<sup>122</sup> Mnajua wakati mtu kweli anapolifuata Neno la Mungu, wakati mwingine kwa ulimwengu anatenda kipumbavu. Ungeweza kuwazia mzee akijenga safina, amesimama pale akijenga safina? Ilikuwa ni upumbavu kwa ulimwengu.

<sup>123</sup> Na kama nilivyosema, mzee mmoja sasa, hapa, mwenye umri wa miaka themanini, ilionekana kana kwamba kama Mungu atamtumia, Yeye angalimtumia alipokuwa mvulana mdogo, mwenye nywele za mawimbi, ama alipokuwa katika kiwango

bora kabisa katika elimu yake. Ilichukua miaka arobaini kuiondoshia hiyo kutoka kwake, ili Yeye aweze kumtumia, ilichukua miaka arobaini kutoa kutoka kwake kile Farao, na elimu yake, alikuwa ameweka ndani yake.

<sup>124</sup> Ilichukua miaka mitatu kwa Mungu kuiondoa kutoka kwa Paulo, huko chini Arabuni, kumrudisha kwa Mungu, ikamrudisha kwenye Neno, kati ya yote. . . kutoka kwa theolojia yote kuu, kadiri ilivyokuwa nzuri, ile theolojia aliyojifunza kwa Gamalieli.

Na kadiri theolojia yake ilivyokuwa nzuri, ambayo yeye, Musa, alijifunza kutoka kwa Farao, hata hivyo, ilimchukua Mungu miaka arobaini kuitoa yote kwake.

<sup>125</sup> Asubuhi moja wakati Mungu aliponena naye, kesho yake asubuhi akawa mshenzi kwa watu. Hebu Mungu aseme na mtu yeyote, na machoni pa ulimwengu wanakuwa wendawazimu. Nami simaanishi m—mlokole, ninamaanisha mwanamume au mwanamke imara anayemjia Mungu, Yeye anakuondolea ushupavu wa dini.

<sup>126</sup> Sasa, tunaona ya kwamba Musa, kesho yake asubuhi, huyu hapa, huku mke wake ameketi juu ya nyumbu, naye maskini mvulana wake, Gershomu, kwenye nyonga yake, na maskini fimbo iliyopinda mkononi mwake, huyu hapa akishuka kwenda Misri kuiteka. Kama nilivyosema “uvamizi wa mtu mmoja” akishuka kwenda kuiteka.

“Kwani unaenda wapi, Musa?”

“Nashuka kwenda Misri.”

“Unaenda kufanya nini?”

“Kuiteka.”

“Utaiteka na nini?”

“Fimbo hii.”

“Ni nani aliyesema hivyo?”

<sup>127</sup> “Mungu alisema.” Amina, hilo latosha. Alikuwa na hakika tu na hilo kadiri alivyoweza kuwa, kwa fimbo hiyo ya kale iliyokauka. Lakini maskini fimbo hii kavu mikononi mwa Mungu, ina maana zaidi ya kila bombomu ambayo ungeweza kuelekezewa. Naam. Maskini mvulana mmoja mdogo, asiye na maarifa, asiye na elimu huko nje mikononi mwa Mungu, asiye na hata elimu ya kutosha kujua ABC zake, angeweza kuleta nguvu zaidi za Mungu kutoka Mbinguni, kuliko madaktari wote wa theolojia walioko katika Marekani hii. . . ?. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

<sup>128</sup> . . . kusahau theolojia yake yote. Haikumbidi kupiga msasa chochote. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Mungu. Naye alikuwa na hakika ilikuwa ni Mungu. Alikuwa na hakika kwamba atawakomboa. Atawalishaje watu milioni mbili na

nusu bila hata chakula? Kundi la watumwa huko nje nyikani, atafanyaje jambo hilo? Alikuwa na hakika Mungu angefanya jambo fulani kulihusu.

<sup>129</sup> “Ndugu Branham, unapohubiri uponyaji wa Kiungu, kuna watu walio na ugonjwa wa moyo, hii . . . Utafanyaje—utalifanyaje litende kazi?” Mimi si . . . si kazi yangu kulifanya litende kazi, hiyo ni kazi ya Mungu kufanya hivyo. Lakini kwa hakika tu kadiri nijuavyo Neno Lake ni kweli, Yeye alimtuma Malaika huyo na kusema hivyo, na mahali fulani humu ndani, mtu fulani ataponywa, nina hakika tu na jambo hilo kama nilivyosimama hapa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Kitu fulani kitatukia, kwa sababu Yeye alisema hivyo. Sijui ni nani, kiko wapi, bali kitatukia. Ni nani? Sijui, si kazi yangu ni nani.

Mtu fulani ataokolewa. “Unajuaje?” Mungu amesema hivyo, nina hakika nalo, nina hakika nalo.

“Vema, Ndugu Branham, umekuwa na mapambano mabaya sana, nilifikiri ulisema Bwana alikuongoza huku.” Aliniongoza.

<sup>130</sup> “Unafikiri ni kitu gani chema kitakachotoka kwake?” Sijui, lakini nina hakika Yeye alinituma hapa, nina hakika ya kwamba Yeye anafanya jambo fulani, sijui ni nini, bali nina hakika Yeye analifanya, kwa sababu ni Neno Lake. Hakuna kubahatisha, najua ni kweli.

<sup>131</sup> Wakati Ibrahimu, mtu mwenye umri wa miaka sabini na mitano, na mkewe sitini na mitano, Mungu alikutana naye siku moja, na kusema, “Ibrahimu, nitakupa m—mtoto kwa mkeo, Sara,” alikuwa tasa, naye ni mgumba, nadhani, nao hawa hapa, baada ya miaka hii yote, vema, kama Mungu . . . Vema, Ibrahimu alikuwa na hakika tu kwamba atampata mtoto huyo kama chochote kile.

<sup>132</sup> Ninaweza kumwazia akisema, “Sara, shona lundo la vijibuti, na ukipatie taulo chache za jicho-la-ndege na pini za nepi, na hebu tuanze, Tunajitayarisha, tutampata.” Vema, linasikika la kipumbavu.

Vipi kama alishuka kwenda kwa daktari, na kusema, “Daktari, mimi na mke wangu, tunataka kufanya maandalizi hospitalini tukapate mtoto?”

<sup>133</sup> Daktari angesema, “Loo, loo, bila shaka, Bw. Abram. Naam, bwana. U-huh.” Aseme, “Aisee, waweza kumwendea . . . waweza kumwita mtaalamu wa magonjwa ya akili, ama wodi ya saikolojia, mahali fulani? Mzee huyo amerukwa na akili.” Lakini alikuwa na hakika Mungu alikuwa anaenda kufanya jambo hilo.

Siku ishirini na nane za kwanza, “Unajisikiaje, mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Utukufu kwa Mungu, nina hakika tu kama nilivyokuwa mara ya kwanza!”

Miaka mitano ikapita, “Unajisikiaje, mpenzi?”

“Hakuna tofauti hata kidogo. Nina umri wa miaka sabini sasa.”

Naam, naye Ibrahimu ana themanini, hilo linaninii . . . “Nina hakika tu kama jambo lolote lile itatendeka.”

Miaka ishirini na mitano ikapita, sasa mke ana tisini naye mume ana mia moja, “Unajisikiaje, mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

<sup>134</sup> “Utukufu kwa Mungu, tutampata haidhuru.” Kwa nini? Alikuwa na hakika ya kwamba Mungu hutimiza Neno Lake. Alikuwa ameshawishika kabisa ya kwamba Mungu aliweza kutimiza yale aliyokuwa ameahidi. Hakika, una hakika wakati Mungu anapokufunulia.

<sup>135</sup> Kama Mungu angemfunulia maskini msichana huyo aliyeketi hapo, angetembea, ninaweka dau ibilisi angeweza kumtuma kila pepo aliye naye, kutoka kuzimu, hilo lisingeweza kulizuia. Mtu huyo aliyeketi hapo kwenye kiti cha magurudumu, hata uwe nani, haingekuzuia. La, hakuna kitu kinachoweza kukuzuia wakati Mungu alisema hivyo, hilo lilitosha.

<sup>136</sup> Huko Ufini, wakati mvulana huyo mdogo alipokuwa amelala pale sakafuni, amekufa:

<sup>137</sup> Ninayo hayo katika maandishi na yametiwa sahihi, ikatangazwa kuwa amekufa, wakaenda wakawachukua mama na baba, kabla mzishi hajaweza kumchukua. Alikuwa amelala pale, nami nikashuka, nikasema, “Huyo ndiye yule mvulana mdogo niliyemwona miaka miwili iliyopita huko Marekani.”

<sup>138</sup> Hapo walisimama yapata watu mia tano, meya wa mji, nilimwambia Bibi Isaacson, “Fasiri hili.” Akafasiri. Nikasema, “Kama mtoto huyo mchanga hatafufuka kutoka hapo alipokufia . . .” Amelala pale amekufa, kila mfupa mwilini mwake umevunjika, ulimzungusha namna *hiyo*, na kumtupa nje, hata mi—miguu yake midogo na kadhalika ilipitia kwenye soksi zake, na viatu vyake vimentoka, na kila kitu. “Kama mtoto huyo mchanga hatakuwa amesimama kwa miguu yake katika dakika tano tangu sasa, mimi ni nabii wa uongo na mwongo, basi nifukuzeni kutoka nchi hii.” Kwa nini? Nilikuwa na hakika huyo alikuwa ni Mungu aliyenionyesha hilo ono. Haina budi kuwa hivyo, hakuna kitu kinachoweza kulizuia. Amina.

<sup>139</sup> Usiku huo huko India, mbele ya watu hao wote, huku Maraja kwenye mito yao, na watu watakatifu wameketi pande zote, nami nilikuwa katika hekalu la Makalasinga na Wajaini siku hiyo, nao wakaudhihakiki Ukristo, Kasema, “Wazo lenyewe,” kasema, “la Kristo kufa!” Wakati hata hawatamwua kiroboto, wanapangusa sakafu wanapoenda, wasije wakamkanyaga chungu, wakihofia kwamba, wanaamini

katika kuzaliwa upya katika mwili wa kiumbe mwingine, wanafikiri huenda akawa ni baadhi ya jamaa zao, ungewezaje kuwahubiria juu ya dhabihu ya Damu?

<sup>140</sup> Nikasema, “Acha Mungu anene, huyo ni Mungu. Baadhi yetu hatuna budi kuwa tumekosea.” Nilichukua Kurani kwa mkono mmoja, Biblia katika huo mwingine, nikasema, “Kuna kasoro mahali fulani. Acha Mungu aliye Mungu halisi anene.” Haleluya!

<sup>141</sup> Yapata wakati huo wakamleta kipofu mmoja huko juu, nikasema, “Siwezi kumponya huyo mtu, bila shaka siwezi.” Nikasema, “Jina lake linaendelezwa R-a-j-a-p-h-e-w,” namna hiyo.

“Hiyo ni kweli.”

Nikasema, “Yeye ni ombaomba. Mke wake ni mwanamke mdogo, mwembamba. Ana wavulana wawili, mmoja wao ana umri wa miaka sita, na huyo mwingine ana minane.”

“Kweli.”

Huku nimesimama huko nje na huo upako, hao Maraja wameketi huko nje, nao hao watu watakatifu wakasema, “Anasoma mawazo yao.”

<sup>142</sup> Nikawaza, “Loo, wanafiki hao!” Ndipo nikaangalia nyuma, nami nikawazia, “Mungu, laiti ungefanya tu jambo fulani!” Nikaangalia nyuma, hili hapa ono, hapo alisimama akiangalia kote, katika ono. Loo, ndugu! Sasa! Sasa hebu jambo fulani litukie! Nikasema, “Nampa changamoto kila shehe wa Kiislamu humu ndani, kila kasisi wa Buddha, ninyi Makalasinga, na Wajaini mlioudhihaki Ukristo, aje hapa, na kumfungua macho yake. Hakika Mungu aliyemwumba, kama wewe. . .”

Akasema, “Nitamtumikia Mungu ayafunguaye macho yangu.”

<sup>143</sup> Nikasema, “Loo, bila shaka, mnasema amekosea, yeye ni mwabudu jua, hakika, yeye anaabudu kiumbe badala ya Muumba.” Nikasema, “Mngeninii. . . Ninyi Wajaini mngefanya nini? Mngemwongoa tu, na kumfanya Mjaini. Ninyi Waislamu mngefanya nini? Mngefanya jambo lile lile. Ninyi Mabudha mngefanya nini? Jambo lile lile; saikolojia tu.

<sup>144</sup> “Tuna kitu kile kile Marekani.” Nikasema, “Wamethodisti wote wanataka kuwafanya Wabaptisti wote, Wamethodisti, nao Wapentekoste wanataka kuwafanya Wamethodisti wote, Wapentekoste, na ni—ni saikolojia tu. Hivyo tu.” Lakini nikasema, “Hakika, Mungu aliyemwumba,” haleluya, “Mungu aliyemwumba anapaswa kufanya jambo fulani kulihusu.”

<sup>145</sup> Vema, mnafikiri ningesema hivyo? Si kwa vyovyote vile, kama sikuwa nimeona ono hilo. Nilijua ni wapi. . . kile kingetukia wakati huo. Ibilisi asingeweza kufanya lolote kulihusu wakati huo.



146 Kama Yeye angeonyesha ono kwamba George Washington atafufuka kutoka kwa wafu asubuhi, ningevalika ulimwengu mzima usimame, uangalie likitendeka, kwa kuwa ni Neno la Mungu. Nimeona maono hayo kwa muda wa miaka hamsini na miwili, wala hakuna hata moja limewahi kushindwa maishani mwangu mwote. Ni Mungu! Hakuna mashaka juu yake, ni hakika.

147 Nikasema, “Sasa, ninyi Waislamu mnaosema ninyi ndio dini kuu kuliko zote, njoni mkayafungue macho yake, nami nitakuwa mwanafunzi wenu. Ninyi Wabudha, njoni mkayafumbue macho yake, nami nitakuwa mwanafunzi wenu. Enyi watu watakatifu, njoni mkayafumbue macho yake.” Huku makumi ya maelfu mara maelfu, wamelala kwenye uwanja huo mkubwa namna hiyo. Hapo aliketi meya wa jiji, nina jina lake na anwani, ukitaka kumwandikia, kumwuliza.

148 Hapo wakasema... Nikasema, “Kwa nini usininii...?” Nikasema, “Ninyi ni umati mtulivu sana. Kwani mna shida gani? Mlikuwa mkiniambia leo jinsi Ukristo ulivyokuwa duni, jinsi dini yenu ilivyokuwa kuu.” Nikasema, “Angalieni ninyi watu huko nje, waangalieni makasisi wenu. Kwani wana shida gani? Waliniita mshupavu wa dini, Mmarekani mwuza sanduku la sabuni, nikiuza dini kana kwamba nilikuwa nimesimama kwenye sanduku la sabuni, maana niliitikisa mikono yangu wakati Roho Mtakatifu alipokuwa juu yangu.” Nikasema, “Hebu wajitokeze basi, na kuyafungua macho ya mtu huyu.” Haleluya!

149 Nikiangalia ono hilo, nikasema, “Kwa nini msije? Kwa sababu hamwezi. Wala mimi siwezi, ila Mungu wa Mbinguni, aliyemfufua Mwanawe, Kristo Yesu, ambaye amenipa ono sasa hivi, ambapo niliona ya kwamba mtu huyo alikuwa amesimama hapa akiwa na macho yake, nilimwona katika ono, kama Yeye hatayafungua macho yake basi mimi ni nabii wa uongo, basi mnifukuze India. Kama akiyafungua macho yake, ni wangapi wenu Waislamu, Wabudha, na ninyi nyote, mtakaompokea Kristo kama Mwokozi wenu?” Mikono myeusi mitupu tu umbali ungeweza kuona.

150 Kasema, “Mleteni hapa.” Nikamkumbatia, nikasema, “Bwana Yesu,” mara niliposema hivyo, akaanza kupigia mayowe *kitu fulani* namna *hiyo*, angeweza kuona vizuri kama nilivyoweza. Akakimbia na kumnyakua meya wa huo mji, akikimbia huku na huku namna *hiyo*. Ilikuwa ni kitu gani? Ni Mungu yeye yule. Neno la Mungu ni halisi tu usiku wa leo kama lilivyowahi kuwa. Hata amemshuhudia rais.

151 Oktoba hii ijayo, wana uwanja mkuu sana wa michezo ambao unaweza kuenea watu milioni ndani yake, huko New Delhi, ambako wanafanyia mkutano wao mkubwa, na wanataka kuja.

152 Hakika, Yeye angali ni Mungu. Lakini unaninii... Huwezi tu kulisema kwa sababu ati unaliwazia niani mwako, huna budi

kulijua, huna budi kujua. Neno halina budi kukuja, huna budi kujua ya kwamba ni kweli.

<sup>153</sup> Maskini Eliya siku ile alipochukua dhabihu hizo zote, na kusema, “Hebu na tuthibitisha ni nani aliye Mungu.” Kasema, angalieni kama alikuwa na hakika juu yake, alisema, “Ni—ninyi tangulieni kwanza.” Kasema, “Ni—ninyi, mko wengi sana, mko makuhani mia nne hapa,” kasema, “ninyi toeni dhabihu, na Mungu anayejibu kwa Moto, na awe Mungu.”

<sup>154</sup> Nao walikuwa waaminifu, hawakuwa wanafiki. Kasema, waliikata-kata hiyo dhabihu, kisha wakapanda juu ya madhabahu, Eliya akazunguka-zunguka, akasema, “Aisee, labda ana shughuli. Huenda amelala kidogo.” Shida ilikuwa ni nini? Alikuwa na hakika, ndugu, alikuwa ameona ono, alisema hivyo.

<sup>155</sup> Ndipo alipochukua na kumwaga maji yote juu ya madhabahu, alisema, “Bwana Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na wa Israeli,” jina lake la kifalme, si—si jina lake la mdanganyifu, “Ibrahimu, Isaka, na wa Israeli, na ijulikane leo hii ya kwamba Wewe ni Mungu, nami ni nabii Wako, nami nimefanya haya yote kwa amri Yako.” Amina. Haleluya! Unapotimiza masharti ya Mungu, itisha Moto, nao utashuka. Hiyo ni kweli.

<sup>156</sup> Hebu kanisa la Kipentekoste lisahau tofauti zao za kimadhehebu, acha watu hawa wajitupe kwa machozi madhabahuni, na hebu watu hawa waje kwa nia moja, mahali pamoja, na waanze kumlilia Mungu, na kusahihisha mambo, kutakuwako na Pentekoste nyingine itakayotukia, na nguvu za Mungu zitalitikisa hili taifa.

<sup>157</sup> Lakini huna budi kufanya hivyo kwa amri Yake. Huwezi kulifanya maadamu unasema, “Vema, ninajua ni—ninapaswa kuamini jambo *hili*, lakini kwa kweli, Biblia inasema *hivi*, lakini mimi. . .” Ah, uh-uh. Yeye ni. . .Kwanza kabisa tayari umeshindwa. Unaona? Unaona? “Vema, najua kanisa letu linasema siku za miujiza zimepita, lakini kwa kweli, ninaamini hazijapita.” Unaona? Umeshindwa, kamwe hutafika mahali popote namna hiyo. Hiyo ni sauti isiyojulikana, hujui la kufanya.

<sup>158</sup> Kuwa na hakika. Ni Neno la nani lililo la hakika? La Mungu. Kama kanisa lako likisema siku za miujiza zimepita, Biblia ilisema, “Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe kweli,” alisema Mungu.

<sup>159</sup> Sauti hiyo haina uhakika, “Peana mikono na mhubiri, mpe mkono wa kuume wa ushirika, kisha uje ukakiri.” Ibilisi alifanya jambo lilo hilo, aliamini ya kwamba Yesu Kristo alikuwa ni Mwana wa Mungu, aliamini kabisa.

<sup>160</sup> Kaini alijenga madhabahu, na kuabudu tu kama vile mtu mwingine yeyote wa kidini alivyofanya, alitoa dhabihu, na kufanya ninii kuu. . .akaweka pesa zake madhabahuni, mali yake, na—na kulala chini kwa uaminifu, na kumwinulia Mungu

mikono na kuabudu. Mungu akamkataa kabisa. Hiyo ni kweli. Huna budi kuwa na hakika, ndugu, inakubidi kujua Mungu ndiye anayenena. Alifanya hivyo kwa mawazo yake mwenyewe, Habili alifanya hivyo kwa ufunuo wa Kiungu wa Mungu, akasiliza Neno la Mungu. Lakini wakati kila kitu kilipokuwa sawa . . .

<sup>161</sup> Daudi, alikuwa na hakika. Akaenda kule siku moja, na maskini yule Goliathi amesimama huko nje, akisema, “Siku za miujiza zimepita, zote zimekwisha. Hebu baadhi yenu . . .” Loo, ibilisi anapodhania amekuzidi kidogo, ndugu, anaweza kujigamba na kujisifu kupita kiasi. Naam, anaweza. Akisimama huko nje, alisema, “Hebu niwaambie, hebu baadhi yenu wanaume huko, baadhi yenu wanatheolojia, mje huku na kunishambulia. Mnaona, nitawaambia nitakalofanya!” mwajua.

<sup>162</sup> Lakini siku moja, alisema hivyo wakati mbaya, ilitokea kulikuwa na jamaa mdogo, mwekundu, maskini jamaa mdogo mwenye mafundo, amevaa koti dogo la ngozi ya kondoo, amejifunika pale, labda yapata, ana uzito wa yapata ratili mia moja na kumi, nywele zikining’inia machoni mwake, kasema, “Kwani ni nani huyu huko, anayeyatukana majeshi ya—ya Neno la Mungu aliye hai? Ni nani huyo huko anayesema hivyo?”

“Loo, huyo ni Goliathi.”

<sup>163</sup> Akasema, “Kwani mtasimama na kuacha dhehebu hilo lisilotahiriwa liseme ya kwamba siku za miujiza zimepita, wakati Mungu wetu alisema Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele?” Loo, lilimgusa jamaa tofauti. Naam, bwana. Huenda wakapatana, lakini akasema, “Sipatani.”

<sup>164</sup> Wakamvuta mbele ya askofu, Sauli, kasema, “Sasa, hebu nakwambie unachopaswa kufanya, mwanangu, kabla hujaingia katika huduma, itakubidi kuchukua miaka minne ya mafunzo ya chuoni, itakubidi kupata Ph.D. na LL.D.” Naye akasema, “Baada ya kukuwekea hizi zote . . .” Nao wakaiweka juu ya maskini jamaa huyo mdogo, alikuwa mwembamba, asingeweza kuishikilia; hivyo karibu ndivyo tunavyoenenda.

<sup>165</sup> Akasema, “Niondolee upuuzi huu!” Sauli akagundua, upesi sana, ya kwamba fulana yake ya kikanisa haikumkaa mtu wa Mungu. Mafundisho yake ya sharti ya kujibunia, hakuwa akiyainamia. La, bwana. Akasema, “Acha niende na kile ninachokiamini.”

<sup>166</sup> Kasema, “Ngoja kidogo, Sauli, nataka kuzungumza na wewe. Ninajua hili ni kombeo tu, sijui lolote kuhusu maskini hizo . . . jinsi unavyopaswa kusimama, na kusema, ‘*Ah-mina,*’ na jinsi unavyopaswa kufanya *haya* yote, wala sijui lolote kuhusu hayo.” Kasema—kasema “Sikilizeni, ninajua kile—kile ninachozungumzia.”

<sup>167</sup> Kasema, “Siku moja nilikuwa nikichunga kondoo wa baba yangu,” amina, kisha kasema, “dubu akaingia na kumkamata

mmoja, nikamfuatilia kwa kombeo hili, nami nikamrudisha.” Akasema, “Kisha simba akaingia na kumkamata mmoja, na kumtoa nje, mwana-kondoo.” Kasema, “Nilichukua kombeo hili, nikatoka nje na kumbwaga chini, alipoinuka, nikamwua, nikamrudisha huyo kondoo.” Kasema, “Kama Mungu aliyemtia simba huyo mikononi mwangu, na dubu huyo mikononi mwangu, ni zaidi sana vipi atamtia huyo Mfilisti asiyetahiriwa mikononi mwangu!” Amina. Alikuwa na hakika alijua alichokuwa anazungumzia.

<sup>168</sup> Sikilizeni, ni kweli, nasema *yake*, na *hahina*, na *tote*, na *dafuda*, na *pepa* yangu, na labda watu wengi hapa, na mchungaji wenu, huenda wasiwe na Ph., L. maradufu, Q.U.R.S.D. kila namna ya upuuzi kwenye jina lake, bali tunajua kile tunachozungumzia. Kweli. Huenda tukaitwa *watakatifu wanaojifingirisha*, na *wendawazimu*, na *wenye mihemuko sana*, na kadhalika, bali tunajua kile tunachozungumzia. Amina.

<sup>169</sup> Hebu niwaambie, ibilisi, sijali wanahubiri kiasi gani dhidi ya uponyaji wa Kiungu, ni kiasi gani wanasema siku za miujiza zimepita, ninawachunga kondoo wa Baba yangu, kansa ilimchukua mmoja na kukimbia, sina Ph.D. yoyote, bali ninayo i-m-a-n-i, kwa hiyo ninamfuata. Nitamrudisha huyo mwana-kondoo ikiwa Mungu atanisaidia, nitamrudisha. Haleluya!

<sup>170</sup> Angalieni kile alichofanya, aliokota mawe matano, hesabu ya neema, Y-e-s-u, [Kiingereza: Jesus—Mfa.] akayaweka mkononi mwake, i-m-a-n-i, i-m-a-n-i katika Y-e-s-u, hili hapa linakuja. Loo, enyi kondoo wadogo, wagonjwa, ninyi ambao ibilisi amewapeleka mahali fulani, na kusema inawabidi kujaza kaburi kabla ya wakati wenu, Ninakufuatilia! Nitawarudisha kwenye malisho ya majani mabichi yenye kivuli, maji matulivu, mle pamoja na kundi lote.

<sup>171</sup> Loo, naam, alijua alichokuwa akizungumzia, alikuwa na hakika ilikuwa ni Mungu, alikuwa na hakika. Hakuna mashaka kuhusu hilo. Kasema, “Ni zaidi sana vipi Mungu atamtia mikononi mwangu!”

<sup>172</sup> Loo, enyi watu, samahani, nilifikiri ilikuwa ni saa moja na nusu. Nipeni dakika kumi zaidi, sivyo? Nitaangalia, nitaweka saa yangu kengele, ikibidi, kama tu mtaninii. . . Nina kengele hapa kwa vyovyote vile, bali ninaona aibu kuiweka. Lakini, ndugu, dada, hii ni kweli. Parapanda ikitoa sauti isiyojulikana. . .

<sup>173</sup> Angalieni, wakati. . . Hebu tumchukue tu mtu mwingine upesi sana. Wakati, Simeoni, alifunuliwa na Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti mpaka atakapomwona Kristo wa Bwana, alikuwa mtu mwenye sifa, alikuwa na Ph.D., L. maradufu D., Q.R.S.T., pia, lakini Roho Mtakatifu akamfunulia, wala hakuona haya, alienda huku na huko akimwambia kila mtu, mzee mwenye umri wa zaidi ya miaka themanini.

Walimdhihakiki, kasema, “Maskini huyo jamaa mwenye mguu mmoja kaburini, huku anateleza na huo mwingine, ati alisema atamwona Kristo!”

<sup>174</sup> Lakini alikuwa, alikuwa na uhakika, alikuwa na haki ya ushuhuda wake, alisema kwa kuwa Roho Mtakatifu alimfunulia. Amina. Alisimama pale, naye akamwona, pia.

<sup>175</sup> Wakati Yesu alipokuwa duniani, Yesu alikuwa na hakika na Neno la Baba, Akasema, “Liharibuni hekalu hili, nami nitalisimamisha tena katika siku tatu.” Sio, “Nitajaribu kulisimamisha, labda litasimama, labda litafanya kazi.” Alikuwa na hakika. Kwa nini? Daudi alisema hivyo, “Sitamtoa Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiacha Nafsi Yake katika kuzimu.” Alijua uharibifu huingia katika siku tatu, mahali fulani katika siku hizo tatu Yeye angefufuka tena, aliamini Neno la Baba. “Liharibuni hekalu hili, nami nitalisimamisha tena katika siku tatu.” “Nitalisimamisha,” sio, “Nitajaribu kulisimamisha.”

<sup>176</sup> Wakati Martha alipomjia, na kasema—kasema, “Ndugu ye—yetu Lazaro, Bwana, kama ungalikuwa hapa, asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atalifanya.”

<sup>177</sup> Akasema, “Mimi ndimi Ufufuo, na Uzima, asema Mungu. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Je, unasadiki haya?”

<sup>178</sup> Akasema, “Naam, Bwana.” “Ah, na—na—nafikiri hivyo, Bwana. Ni—nina hakika kabisa, lakini wananiambia ya kwamba Wewe ni Beelzebuli tu, wananiambia Wewe huyasoma mawazo ya watu.” Huh-uh, lisingetukia. “Naam, Bwana, naamini,” (Utukufu kwa Mungu!) “Ninaamini ya kwamba Wewe ndiye Mwana wa Mungu aliyekuwa aje ulimwenguni.” Loo, loo, jambo fulani halina budi kutukia. Sikilizeni, hilo ni hakika, hilo ni hakika! Wakati mikataa miwili ya moja kwa moja inapokutana, jambo fulani halina budi kutukia. Loo, naam. Loo, hakika linatukia. Kasema, “Ninaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu aliyekuwa aje ulimwenguni.”

<sup>179</sup> Yesu alimwambia nini? Yeye alisema nini? “Vema, niwaambie nini, mmemzika wapi? Nitashuka niende kule, nijaribu kuona kile ninachoweza kumfanyia.” Uh-um. “Nitashuka niende nikamwulize Baba nione atakalofanya.” Loo, la, uh-uh, Yeye hakusema hivyo. Alisema, “Nitaenda nikamwamshe.” Hakuna kitu kisicho na hakika kuhusu hilo. “Nitaenda nimwamshe.” “Nitaenda,” si, “Nitaenda nikajaribu,” “Nitaenda.” Alijua yale hasa Mungu alikuwa amemwonyesha, Naye alijua litatukia. “Nitaenda nikamwamshe.” Hakuna sauti isiyojulikana katika hilo, la, bwana, hakuna mashaka hata kidogo kuhusu hilo.

<sup>180</sup> Loo, “Uharibuni mwili huu, nitaufufua katika siku tatu.” Yesu alisema, “Kama Mimi...Mkiwa ndani Yangu,

na Neno Langu ndani yenu, mnaweza kuomba mtakalo, nanyi mtatendewa.”

“Hu—huenda labda utatendewa”?

La, la, hakuna mashaka kuhusu hilo. “Nitafanya hivyo. Itatendeka. Itatendeka.” Hiyo ni kweli?

<sup>181</sup> Alipouangalia ule mtini na kuulaani, na saa ishirini na nne baadaye akapitia hapo, nao ulikuwa umenyauka, Petro akasema, “Tazama, ule mtini tayari umenyauka.”

<sup>182</sup> Yesu akasema, “Mwaminini Mungu. Kwa maana amin, amin, nawaambia *ninyi*, kama *ninyi*,” sio *Mimi*, bali *ninyi*, amina, ndugu, “*ninyi* mkiuambia mlima huu,” si, “kama nikisema,” bali, “kama *ninyi* mkiuambia mlima huu, ‘Ng’oka, ukatupwe baharini,’ wala msitilie shaka, bali mwamini ya kwamba hayo mliyosema yatatimia, yatakuwa yenu.” Amina. Si, “labda mtafanya hivyo,” si, “labda mtafanya hivyo,” bali, “mtafanya.”

<sup>183</sup> Ewe mtu mwenye dhambi, nilichora picha hii nyeusi hapa mwanzoni mwa mahubiri yangu, kuhusu saa tunayosimama, hebu niwanukulie Neno, wazieni hilo, Yohana Mtakatifu 5:24, konzi tano, dazani mbili za mayai, lisome utakapoenda nyumbani, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka...” Kama taifa lako linavunjika, kama nyumba yako inavunjika, kama mishipa yako inavunjika, kama afya yako inavunjika, kama matumaini yako yanavunjika, kila kitu kinavunjika, lakini Yesu Kristo alisema hivi: “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Haleluya! Si, “Huenda,” “Atapita, amepita,” “Huenda katika siku zijazo,” bali, “Amepita sasa.” “Amepita kutoka mautini kuingia Uzimani,” naye yu hai, sasa hivi.

<sup>184</sup> *Whoo!* Laiti ningalikuwa mara mbili ya ukubwa wangu, labda ningejisikia vizuri maradufu ya hivi; Ingenibidi kuwa mara mbili ya ukubwa wangu kufanya hivyo. Ee Mungu, ninawezaje kamwe kukushukuru? Naam, bwana.

<sup>185</sup> Hakika! Kote katika nyakati Yeye hajabadilika kamwe. Maskini Kanisa hilo dogo lililoamini hilo, Neno hilo la Mungu, limepitia kwa shida moja kwa moja katika kila mateso, wamejaribu kuliangamiza kabisa, kulichoma moto, kulitesa sana, kuliua, kulizamisha, Nalo linasonga mbele kwa shida.

<sup>186</sup> Wakati fulani uliopita, nikisimama kwenye ile Sanamu ya Uhuru, kundi dogo la shomoro, ambao, wamelala maiti. Nikasema, “Kwani kuna nini?”

<sup>187</sup> Kasema, “Kuna dhoruba jana usiku, nayo hiyo taa kubwa ilikuwa ikimulika sana, nao maskini ndege hao walikuwa wamepotea. Laiti wangejua tu kutumia taa hiyo, wangeweza kwenda kwenye usalama.” Lakini kasema, “Walikuwa

wakijaribu kufanya nini? Walikuja hapa mbio, na kujaribu kuipiga hiyo taa izimike.” Kasema, “Walifanya nini? Walipiga bongo zao wakijaribu kuzima taa, taa ambayo ingeweza kuwasaidia.”

<sup>188</sup> Enyi Wapentekoste baridi, wa kawaida; ninyi Wamethodisti baridi, wa kawaida; ninyi Wabaptisti baridi, wa kawaida; wewe usiyeamini, unayejaribu kumtoa Kristo humu nchini, ukijaribu kuweka elimu na sayansi badala ya Roho Mtakatifu, utapiga bongo zako zitoke, nayo Nuru ingali itaangaza, na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea. Atakuwa na Kanisa lililojazwa na Roho Mtakatifu ambalo atalijia, Naye ataishi na kutawala ndani Yake. Kamwe hamtalishinda, mnaziharibu tu akili zenu, huku mkisoma vitabu vya kujibunia vya mafundisho ya sharti ya kila namna, lichukueni Neno la Mungu na kulisoma, na mseme ni la kweli, na kulikubali. Hakika.

<sup>189</sup> “Yeye aniaminiye Mimi,” Yohana Mtakatifu 14:7, “Yeye aniaminiye Mimi kazi nizifanyazo, labda naye atafanya zile zile.” Hilo lingekuwa lisilo na hakika *sana*, sivyo? Lakini, “yeye atafanya, atafanya kazi zile zile nizifanyazo Mimi, na nyingi kuliko hizi, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba Yangu.” Hakuna mashaka juu yake, ni hakika.

Unasema, “Lakini, Ndugu Branham, nime—nimejiunga na makanisa yote.”

<sup>190</sup> Kwenye Siku ya Pentekoste, kama nilivyosema jana usiku kuhusu Daktari Simoni Petro, Petro alisema, “Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi *mtapokea* kipawa cha Roho Mtakatifu.” Sio, “ninyi, labda, mtapokea, labda, mtapokea,” bali “mtapokea kile Kipawa, Roho Mtakatifu. Kwa maana ahadi hii ni kwa kizazi hiki, na ni hayo tu”? Loo, la. “Kwenu ninyi, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Sio, “labda,” bali “wote watakaoitwa na Bwana Mungu, mtampokea Roho Mtakatifu.”

<sup>191</sup> Shida yake, mnataka kupeana mikono na kunyunyizia, badala ya kutubu na kubatizwa. *Tubu* maana yake ni, “geuka.” Acha kutokuamini kwako nyuma, anza safari barabarani ukimwamini Mungu, kuelekea Kalvari. Geuka, anza safari, nawe utapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, utapokea.

<sup>192</sup> Hiyo ni kweli, ndugu? Sikunukuu Maandiko hayo vibaya, sivyo? Nimeyaweke jinsi tu yalivyoandikwa. “Mtapokea Roho Mtakatifu.” “Mtapokea,” si “labda, labda mtapokea, mnapaswa kupokea,” bali, “mtampokea. Vema, ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Hilo ni hakika.

<sup>193</sup> Sasa, usiende tu huku, na kusema, “Ninaamini ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu,’ nishikilie kichwa changu juu, na kutikisiwa chumvi, nimwagiwe matone machache ya maji. Nirudi, na kusema, ‘Mimi ni mfuasi kamili sasa, nimepewa mkono wa kuume wa ushirika.’” Kamwe hutampata Roho Mtakatifu, huna chochote, mchafuko mtupu. Hiyo ni kweli.

<sup>194</sup> Toa ulimi wako, kula mkate mwembamba kidogo ambao ulitengenezwa na mtu fulani, kisha kasisi anakunywa divai, kasema, “Nilikula ushirika mtakatifu, ekaristi takatifu,” ambalo linamaanisha *Roho Mtakatifu*, Roho Mtakatifu hakuja na mkate mwembamba, alikuja kama sauti kutoka Mbinguni, kama upepo wa nguvu ukienda kasi, iliyojaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kweli. Mnaona? Hilo halina uhakika. Siwezi kusoma *hilo* katika Biblia. Lakini ninapomsikia akija kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, ndivyo hivyo. Kweli.

<sup>195</sup> Yesu alisema, “Ngojeni huko juu, hadi Yerusalemu sasa. Msianze kuhubiri, msininii. . . Sijali una ujuzi kiasi gani, na umepitia seminari ngapi, na umehitimu umbali gani, ngoja huko juu *mpaka*.”

“Mpaka nini? Mpaka tutakapopata Digrii yetu ya Sanaa?”

“La, bwana. Ngojeni *mpaka*.”

“Siku mbili?”

<sup>196</sup> “*Mpaka* mtakapovikwa uwezo utokao Juu. Halafu, wala si hapo kabla, mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, Uyahudi,” na Bloomington, Illinois, mahali popote, pande za mwisho za dunia. Hiyo ndiyo Injili.

<sup>197</sup> Na kwa hiyo, wakasema, “Sasa, tutapanda tuone kama askofu atakuja.” Hivyo ndivyo tunavyofanya siku hizi. “Loo, tutaona kama kasisi atatupa, uh, atatupa kipa imara.” Hiyo ilikuwa ni sauti isiyojulikana, sijui lolote kuihusu, mimi ni kama Daudi, “Nivue maskini silaha hiyo.”

<sup>198</sup> “Vema, kama utaenda shuleni na kujifunza,” si—sijui lolote kuhusu hilo pia, mnaona, sijui lolote kuhusu hilo. Biblia haisemi lolote kuhusu hilo, kamwe sioni lolote katika Biblia kuhusu hilo.

<sup>199</sup> “Vema, sasa sikilizeni, kama utakiri kwa midomo yako ya kwamba Yesu ndiye Kristo, na kumchukua Yeye, umempokea Roho Mtakatifu, maana mara unapoamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, unaye Roho Mtakatifu.” Hiyo ni sauti isiyojulikana. Hiyo ni kweli.

<sup>200</sup> Paulo alisema, baada ya kuona watu hata waliokuwa wameokoka, na kupaza sauti na kuruka-ruka, alisema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?” Matendo 19:5. Loo, naam, aliwauliza. Naye alisema, “Kama Malaika kutoka Mbinguni,” sembuse mhubiri, “kama Malaika kutoka Mbinguni, akiwahubiri ninyi Injili yoyote isipokuwa hii



ambayo nimekwisha kuwahubiri, na alaaniwe.” Hakuna sauti isiyojulikana kuhusu hilo, hiyo ni Biblia, bila shaka.

<sup>201</sup> Basi wakati wote walipokuwa huko juu mahali pamoja, na nia moja, na ghafla ikaja, si sauti isiyojulikana, la, lakini sauti dhahiri ikaja, na kuijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi, Ndimi zilizogawanyika zikawakalia kutimiza unabii wa Isaya 28:19, kwamba Roho Mtakatifu aliketi juu yao, na wote wakaanza kunena kwa lugha kama Roho alivyowajalia kunena.

<sup>202</sup> Hebu kidogo. Waebrania 13:8 ilisema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” “Kwa sehemu ni yeye yule jana, leo, na hata milele”? Yeye *ni* yule yule, hakuna mashaka kuhusu hilo.

<sup>203</sup> Katika kufunga huenda nikasema jambo hili, mimi huwaweka muda mrefu sana, najua mimi huwaweka, lakini loo, enyi maskini vichwa vyenye usingizi ambao inawabidi kutoka nje na . . . Wakati walikuwa wakiomba usiku kucha na . . . Ni vigumu sana sasa. Tafadhali msifikiri ninawaudhi, ninafuata tu yale Yeye asemayo niambiwe, maana sijui la kusema, Sina ujasiri wa kutosha kusema hivyo, bali nina ujasiri wa kutosha tu kusema yale Yeye asemayo niseme, halafu ni juu yenu.

<sup>204</sup> Angalia, ni wangapi waliopata kusikia habari za Paul Rader? Aliandika wimbo huu maarufu, *Amini Tu*. Paul alikuwa ndugu mzuri sana, nilimjua. Alikuwa ni mtu wa mwituni, alikuwa anakata miti.

<sup>205</sup> Naye akasema, wakati mmoja alipokuwa katika huduma za kimishenari, alishikwa na ugonjwa, ninaamini alikuwa na homa ya maji meusi, ama kitu fulani. Yeye na mkewe walikuwa huko chini visiwani, nao walikuwa mbali sana na madaktari na kadhalika. Naye Paul, mtu yeyote aliyemjua Paul, alijua alikuwa mwaminio wa uponyaji wa Kiungu. Kwa hiyo basi . . .

<sup>206</sup> Nitakuwa nikihubiri karibu na maskani yake juma moja baada ya juma lijalo. Jambo lingine, nitakuwa nikihubiri ninii ijayo, juma moja baada ya juma lijalo, katika viunga vya—vya Bloomington, viungani, Chicago, mnaona, vya Bloomington, kwa hiyo njoni huko. Mnaona? Na kwa hiyo basi . . . Kumbukeni, msiwaambie watu wa Chicago hilo hata hivyo, sijui kama wangevumilia hilo ama la, lakini kwa vyovyote vile, nitakuwa huko, Bwana akipenda.

<sup>207</sup> Ndipo basi Paul Rader, alisema alikuwa mgonjwa sana, akazidi kuwa mgonjwa zaidi, zaidi, zaidi. Ndipo giza likaingia chumbani. Akasema, “Mke wangu, njoo karibu.” Kasema, “Mpenzi, huenda ninaondoka sasa.” Kasema, “Simama karibu na kitanda changu, uniombe.”

<sup>208</sup> Kukaendelea kuwa giza zaidi na zaidi, akaendelea kukiri, “Mungu, Wewe ni Mponyaji wangu.” Giza zaidi, na zaidi, zaidi, zaidi, zaidi, zaidi, likaendelea kuongezeka. Baada ya kitambo kidogo akazimia kabisa.

209 Naye akaota, akasema alidhani alikuwa amerudi, alitoka Oregon, mwajua, akasema alidhani alikuwa amerudi huko akikata miti. Naye bosu wake, alikuwa kwenye msitu wa magogo, kasema, “Paul, kwea, ukauangushe mti fulani wa inchi kumi na nane,” ama mti wa inchi kumi na nne, ama kitu kama hicho, “uulete huku chini.”

210 Kasema, “Vema.” Akasema alipanda juu ya kilima, akinusa hizo sindano za ajabu za misonobari, na akiwa tu na wakati mzuri sana. Kasema alichukua. . . “Ungeweza kuhisi maskini shoka hilo likatalo kuwili likizama kwenye mti huo mwororo, mwajua.” Kadiri unavyoenda mbali zaidi kaskazini, ndivyo inavyokuwa baridi zaidi, ndivyo mti ulivyo mwororo zaidi, kadiri unavyokuwa joto zaidi, mbona, ndivyo mti ulivyo mgumu, nyenzo zile zile.

211 Kwa hiyo basi, akasema alikuwa amekata huo mti, akaupogoa upesi sana. Kasema alichomeka shoka lake ndani yake, kasema, “Jamani,” angeunyanyua mti huo, mwajua, Paul alikuwa mtu mwenye nguvu, mwenye uzito wa zaidi, loo, zaidi ya ratili mia mbili. Kwa hiyo, akainama, akaweka magoti yake pamoja, nayo misuli ya mtu iko mgongoni mwake, na miguu yake, na kadhalika, kwa hiyo akainama chini, na, ili aweze kuuinua. Ndipo alipoushika, alivuta, na kuvuta, na kuvuta, wala asingeweza kuuinua.

212 Alikuwa amekwama, naye akasema, “Nimepoteza nguvu zangu, kamwe siwezi kuliinua gogo hilo. Mbona, nimeyabeba ya mara mbili ya ukubwa huo!” Ndipo akajaribu tena, naye akapambana, na kupambana, na kupambana, mpaka akachoka kabisa. Mnaona, ilikuwa hiyo—hiyo homa. Kasema alidhoofika sana, mpaka akaketi tu kuegemea mti, na kusema, “Mimi, siwezi kwenda mbele zaidi, nimekwisha tu, siwezi kwenda mbele zaidi.”

Ndipo akasema mara akasikia Sauti Yake, Bosu wake, Sauti ya Bosu wake, “Paul?”

Naye akasema, “Naam, Bosu?” Kasema, “*Hiyo inasikika tamu sana.*”

Kasema, “Kwa nini kupambana nalo hivi?”

Kwa hiyo akageuka, akasema haikuwa bosu wake, Bosu wake *halisi*.

213 Akasema, “Paul, unapambana tu nalo, na kupambana nalo, na kupambana nalo.” Kasema, “Unaona kile kijito cha maji kilicho papo hapo?”

Kasema, “Naam.”

214 Kasema, “Kijito hicho cha maji kinashuka moja kwa moja hata kambini.” Kasema, “Mbona usilitupe tu mtoni, ulirukie, kisha uende uteremke hadi kambini?”

215 “Loo,” akasema, “sikuwazia hilo kamwe.” Kasema alilisukuma tu majini, na kulirukia. Kasema alipita juu ya mawimbi, akiwa tu na wakati mzuri akiyapiga maji, akisema, “Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake!” Ndipo alipojirudia, alikuwa amesimama moja kwa moja katikati ya sakafu, akipiga mayowe, kwa sauti yake yote, ameponywa kabisa, akisema, “Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake!”

216 Biblia ilisema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Nimepanda juu yake! “Roho Mtakatifu ni kwa ajili ya yeyote atakaye.” Nimepanda juu yake! Ninaamini ya kwamba Yesu Kristo amefufuka katika wafu. Tunaishi katika siku za mwisho, naye Yesu alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya aniaminiye Mimi,” naye akaahidi katika siku hizi za mwisho, ya kwamba ishara hiyo ya Masihi ingerudi Kanisani.

217 Enyi wanatheolojia, tofautianeni nalo mkitaka, nami nitawaelekeza kwenye BWANA ASEMA HIVI, usiku baada ya usiku nimefanya hivyo. Vipi kuhusu hilo? Nimepanda juu Yake, Neno la Mungu. Amina. Hmm! Najisikia kupaza sauti. Nimepanda juu Yake, Neno la Mungu. Ninaamini ni kwa yeyote atakaye, na aje. Mnaona?

218 Ninaamini Yeye yupo papa hapa sasa. Ninaamini ya kwamba kamwe sitaninii... siwezi... Maneno hayo, kama hukubaliani Nayu, yametoka kwa Mungu. Nimepanda juu yake! Nimepanda juu Yake kwa miaka thelathini na moja, na maadamu Bwana atanijalia kuishi, na kudumisha akili yangu timamu, kwa neema Yake, nitapanda juu Yake, mpaka nitakapofika kwenye mto wa Yordani, nitalitupa ndani, na kupanda juu Yake kote kuuvuka. Ninaamini hilo ni Neno la Mungu la Milele, na mbingu na nchi zitapita, bali Neno Lake halitapita kamwe. Amina. Nimepanda juu Yake.

219 Ninaamini huyo ni Roho Mtakatifu aliye humu ndani sasa, ninaamini huyo ndiye Yesu Kristo. Ninaamini huyo ni Yeye yule aliye—aliyewatokea usiku huo, kama kule kunena kwa lugha kulivyosema usiku wa leo, ama, ile tafsiri, wakati walipofungiwa ndani, Yeye alijionyesha Mwenyewe yu hai.

220 Kuna...? Sininii... Billy hajasambaza kadi za maombi, ninaamini, wakati mmoja juma hili, naamini alisema. Nina shaka kama kuna yeyote hapa au la, si lazima hata wawepo. Hatuhitaji kadi yoyote ya maombi, kadi ya maombi ni namba tu ya kukuleta jukwaani. Haikubidi kuingia jukwaani kumwona Kristo, Yeye yuko mahali utakapokutana Naye, moja kwa moja huko nje, mahali ulipo sasa. Ninakusahi ulichukue Neno la Mungu na kupanda juu Yake mara moja, uone kama ni la kweli. Unaliamini?

Ni wangapi wasio na kadi za maombi? Inueni mikono yenu. Wewe ni mgonjwa? Vema, nachani ni kila mahali kwa jumla.

221 Baba wa Mbinguni, loo, njia yangu fidhuli, Bwana, Si—sikapata nafasi ya kuzungumza na ninii, kama wahudumu wanavyonena katika siku hizi za mwisho, Mungu. Sijui ni kwa nini hukuniruhusu kuwa nayo, lakini laiti ningalifanya kile nilicho nacho moyoni mwangu, kuninii tu, ningenena kwa njia ambayo wangelielewa. Tafadhali, Bwana, nijalie kwa rehema za Mungu moyoni mwangu, niwathibitishie ya kwamba jambo ninalojaribu kuwaambia ni kweli, kwa vyovyote vile, Baba. Ninaomba ya kwamba utafanya hivyo mara nyingine tena.

222 Na—nakuomba ufanye hivyo, Bwana, ili watu wajue ya kwamba kama Wewe ulisema hivyo, ni kweli, Mungu, haina budi kuwa ni kweli, wala si sauti isiyojulikana. Kama ulifufuka tena, ulisema ya kwamba Kanisa lako lingekuona, ungekuwa pamoja nao, na kufanya, Ka—Kanisa lingefanya jambo lile lile ulilofanya, Nawe ungekuwa pamoja Nao sikuzote, hata ukamilifu wa dahari. Mungu, ninasimama juu ya hilo, ulilithibitisha, ulisema ulikuwa, nami ninajua Wewe upo hapa usiku wa leo.

223 Basi, Mungu, nisamehe tabia yangu ya kupagawa, mhemko, na wasiwasi. Nami naomba, Baba, ya kwamba utatusamehe dhambi zetu na kutokuamini kwetu, na kwamba Wewe utatutuliza chini ya nguvu za Roho Mtakatifu. Na jalia wanaume na wanawake, mtu fulani humu ndani usiku wa leo, Bwana, awe na imani ya kutosha kukuita ushuke kutoka Utukufuni. Na jalia magonjwa yao na kadhalika yawe hivi kwamba, kama ni makuu, ama kama sivyo. . . Wewe ni Mungu, Wewe unajua mambo yote.

224 Ulimponya mtu aliyekuwa na, namna fulani ya ugonjwa uliodumaa, na kuwaacha mamia wameketi pale wamepindika, viwete, na vipofu, ndipo ukaja na kuwaponya waliopindika, viwete, na vipofu. Wewe ni Mungu tu, Wewe fanya utakacho.

225 Mimi ni mtumishi Wako, Bwana, na hawa ni watumishi Wako walioketi hapa. Ili iweze kulitia moyo kanisa, na ijulikane, usiku wa leo, Bwana. Hebu . . . Tutafunga milango ya—ya kutokuamini kwote na kukuingiza ndani ya moyo wetu, kama Kleopa, na hao wengine, waliotoka Emau.

226 Umezungumza na wengi wa watu hawa, hawa Wamethodisti wazuri, Wabaptisti, Wakatoliki, Wapresbiteri, Wapentekoste, labda hawakutambua ilikuwa ni Wewe, basi, Baba, ninaomba, usiku wa leo, ya kwamba utafanya jambo fulani jinsi tu ulivyofanya kule, mambo tu uliyofanya kabla hujasulubiwa, ili kwamba wajue ya kwamba Wewe ni Bwana aliyefufuka, kwamba Wewe hujafa, Wewe upo hapa, U hai.

227 Wamelisikia sana, Bwana, mpaka linakuwa tu la kawaida kwao, lakini ninaomba, Mungu, ya kwamba usiku wa leo, itakuwa ni mpya kwao, kuwafanya wajue ya kwamba huyu Yesu aliye hai, ambaye yuaja hivi karibuni, yuko hapa miongoni mwetu. Hivi hutafanya hivyo, Baba? Ninaomba kwa ajili ya

utukufu wa Mungu, na kwa ajili ya kulijenga Kanisa Lako, katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>228</sup> Niangalieni kama mtumishi Wake, aminini kwa moyo wenu wote, enyi wagonjwa. Usiwe na shaka hata moja niani mwako, bali amini kwa moyo wako wote, uone kama Yeye anadumu, kama Yesu Kristo yu hai.

<sup>229</sup> Ninaishikilia mikono yangu kwa uchaji mbele za Mungu, ya kwamba watu pekee ninaowajua ambao ningeweza kuwatambulisha katika jengo hili, wala nisingewaambia, ni rafiki yangu hapa, Ndugu Gene Goad, na Ndugu Skaggs kutoka Chicago, anayefanya kazi na Kampuni ya Winchester, yeye ni . . . ana mahali pa michezo, marafiki zangu wa kibinafsi.

<sup>230</sup> Sina hakika kama maskini wanawake hawa wawili, ama watatu, wanaoketi hapa nje, ni marafiki zangu kutoka Chicago. Maskini wasichana hawa wawili walioketi hapa, msichana mwenye nywele nyekundu, msichana mwenye nywele nyeusi, kama, sina hakika, hao ni binti za Ndugu Welch Evans. Hiyo ni kweli?

<sup>231</sup> Nje ya hao, naam, huyu hapa mmoja wa Wafanyabiashara Wakristo kutoka Chicago, siwezi kulikumbuka jina lako, mwanao ndiye katibu, papa hapa, siwezi kukumbuka jina lako. Naam, ninyi wawili pamoja hapo. Hiyo ni . . . Nilikuona tu umeketi hapo.

<sup>232</sup> Kuhubiri, kwa upako huu . . . Sasa, i—ipo hapa, niliihisi. Ninajua karibu inakupofusha, unaona, mpaka wewe si wewe tena. Nje ya hao simjui mtu yeyote, hakuna watu.

<sup>233</sup> Mwaminini Mungu, amini, useme, “Bwana, Yesu, najua Biblia inasema ya kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, nami ninajua ya kwamba Wewe ungali ni yule Kuhani Mkuu.”

<sup>234</sup> Mnasema, “Amina”? Basi kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, mnaamini hilo? Je, uko tayari kupandisha nafsi yako juu ya hilo kutoka hapa hata Umilele, ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? Basi kama Yeye ni yule yule, angetendaje? Kama vile alivyofanya wakati huo. Hiyo ni kweli?

<sup>235</sup> Je, Biblia inasema ya kwamba Yesu ni Neno la Mungu? Tunaamini hilo? Nayo Biblia ilisema ya kwamba Neno la Mungu ni Mpambanuzi wa mawazo ya moyo. Hiyo ni kweli? Basi ombeni. Hiyo si ni changamoto?

<sup>236</sup> Sasa kwenu ninyi mlio na shaka: Mkitaka kuja hapa kwenye maikrofoni hii, enyi wakosoaji, nawe unataka kuchukua maikrofoni hii, na kufanya mambo yale yale, ni yako. Njoo uchukue mahali pangu. Na kama hamwezi, basi tulieni milele. Askofu, paroko, daktari, yeyote yule, njoo ufanye hivyo. Halafu umwamini Yesu Kristo.

Ombeni, ninyi Wakristo.

237 Mnasema, “Unaogopa, Ndugu Branham?” Nina hakika. Nina hakika ya kwamba yule Malaika aliyenena nami usiku huo, aliniambia Neno la Mungu. Siogopi, Yeye atafanya, Yeye aliliahidi.

238 Sasa, siwezi kukuponya. Mtu yeyote anayewazia hivyo, wewe ni—wewe ni—wewe ni—wewe hata si. . . U—unafiki-. . . Ukiweka hilo kichwani mwako, hu—hutaitwa kamwe. Weka kichwani mwako ya kwamba Yesu Kristo tayari amekufanyia hilo, kisha uamini.

Ninangojea tu, si—siwezi, Yeye asiponiambia, siwezi kusema lolote.

239 Ndugu, naomba kwenye piano hiyo, *Amini Tu*, muda kidogo tu kwa ajili ya wimbo. Nimekuwa nikihubiri kwa nguvu sana. Kwa utulivu tu, “Amini tu, amini tu,” kwa utulivu sasa.

240 Hebu tumwazie Yeye akishuka akitembea. Sema, “Bwana, mimi ni mgonjwa mahali pengi, utanirehemu?”

“Ninaweza kama ukiamini, kwa kuwa mambo yote yanawezekana kwao waaminio.”

241 “Ndio kwanza niambiwe ya kwamba Neno Lako linasema *hivi-na-vile*, kwamba Wewe ungekuwa Kanisani Mwako, na kujitambulisha Mwenyewe, kama tu ulivyofanya; nimemsikia akisimulia hilo juma zima. Mimi. . . Hapana shaka huyu mtu anasema kweli, maana ninaenda moja kwa moja nyumbani, nikayasome kutoka katika Biblia, ni ahadi. Labda sikufundishwa hilo, bali ninajua ni kweli. Ninakuamini Wewe, ninakuamini Wewe, Bwana, saidia kutokuamini kwangu.”

242 Sasa hapo, hapo. Katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu.

243 Hapa, inua kichwa chako. Maskini mama huyo mwenye mvi aliyeketi hapo. . . Sina budi. . . papa hapa, yule, maskini mama huyu papa hapa, huyu hapa mama, samahani, si huyu. Inaning’inia hapa.

244 Hivi hamwezi kuiona hiyo Nuru? Angalieni hapa, Nuru ya kaharabu kama mnavyoiona kwenye picha, Hiyo hapo moja kwa moja juu ya huyo mama, inazunguka-zunguka. Samahani kama nikiwauliza hivyo, hiki ni kiwango kingine.

245 Ninatambua ya kwamba niko kwenye jumba la mikutano, nami ninatambua ninamwangalia mwanamke, naye anaomba, nami ninamwangalia. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Lakini ninaweza. . . Kama ningekwambia, kwa Roho Mtakatifu, kile unachoombea, utajua kama ni kweli ama si kweli. Unaombea henia. Hiyo ni kweli. Pia, ugonjwa wa matumbo, matatizo. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako namna *hii*. Kama hatufahamiani, inua mkono wako mwingine juu.

Kuna ishara fulani ya kufufuka Kwake. Aligusa kitu Fulani. Hiyo ni kweli?

Na ninyi nyote je? Mnaamini?

246 Ugonjwa wa mgongo. Sikujui, sivyo? Hatufahamiani. Una shida kwenye uti wako wa mgongo. Vipi kama Mungu angeniambia wewe ni nani? Je, ungeniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Bibi Hollenbach. Hiyo ni kweli.

247 Hiyo ilimsaidia rafiki yako aliyeketi karibu nawe. Sikujui wewe pia, bali Mungu anakujua. Lakini hujiombe mwenyewe, unamwomba mtu mwingine. Kama nikikwambia ni kitu gani, ungeniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unamwomba mpwa ambaye ni mlevi sugu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

Ninakupa changamoto kuamini.

248 Mtu huyu aliyeketi hapa ameinamisha kichwa chake, akilia, akiomba, aliyeketi hapa kwenye vipandio. Una ugonjwa wa tumbo, sivyo, bwana? Wewe ni mgeni kwetu. Unakaa kidogo, huna budi kurudi nyumbani, unatoka Des Moines. Hiyo ni kweli. Mke wako ana ugonjwa wa tezi, sivyo? Mvulana wako mdogo, mtoto mdogo ana ugonjwa wa pumu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Weka mkono wako juu ya wote wawili; amini, kisha uende nyumbani, na uwe mzima.

249 Huna kitu kama kadi ya maombi, sivyo, bwana? Uliamini tu, hiyo ni kweli? Hatufahamiani, inua mkono wako. Mimi na wewe hatufahamiani, hatufahamiani. Amini.

Iweni katika maombi. Nimeona jambo fulani likitukia, sina hakika sana lilikuwa wapi. Aminini, kwa uchaji.

250 Ni mwanamume. Inua kichwa chako, papa hapa ndani. Unaugua ugonjwa wa kibofu nyongo. Ulikuwa ukiomba, "Ee Mungu, jalia iwe ni mimi, usiku wa leo." Hiyo ni kweli, bwana? Je, hatufahamiani? Inua mkono wako kama hatufahamiani. Hivi hamwezi. . . ? Ninajua hamwezi kuiona Hiyo, Nuru ile iliyo juu yake. Hutoki papa hapa, unatoka kwenye mji unaoitwa Canton. Hiyo ni kweli. Jina lako ni Bw. Ellis. Hiyo ni kweli, sivyo? Inua mkono wako. Hiyo ni kweli.

251 Huyu hapa mama mmoja, chini yako tu, ameketi chini huku, mikonono juu kinywani mwake, akiomba, ana ugonjwa wa tumbo. Una ugonjwa wa kikoromeo kwenye koo lako, pia. Hatufahamiani. Aisee, wewe pia unatoka Canton. Hiyo ni kweli kabisa. Jina lako ni Bibi Effland, E-f-f-l-a-n-d. Kama hiyo ni kweli inua mkono wako, ama, simama kwa miguu yako ili watu waweze kuona ya kwamba hiyo ni kweli. Sasa, kama hatufahamiani, inua mkono wako. Unaniamini mimi? Basi ninakupeleka nyumbani ukapate afya, katika Jina la Yesu Kristo.

252 Nimepanda juu Yake! Haliwezi kushindwa, ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliyefufuka katika wafu, akifanya jambo lile lile alilofasiri Roho Mtakatifu kupitia kwa yule mtu, usiku wa

leo, na kusema, “kama walivyokuwa wakitoka Emau, kujifungia pamoja na Mungu.” Unaamini hilo kwa moyo wako wote?

<sup>253</sup> Sasa, wakati inaponipofusha mimi, ni wenye dhambi wangapi humu ndani walio . . . ? Kila mmoja wenu njoni hapa, na msimame karibu nami kwa dakika moja tu. Mnataka kupanda Utukufuni juu ya Neno Lake? Njoo hapa, na usimame hapa kwa dakika moja. Mwingine? Toka kwenye roshani. Simama. Wenye dhambi wote waje hapa kwa dakika moja, vijana kwa wazee. Hiyo ndiyo njia ya kuja. Songeni mbele moja kwa moja. Ni sawa, ndugu. Imani *kama hiyo*, huku watu wakianguka mmoja juu ya mwingine. Njoo. Njoo!

<sup>254</sup> Kwa nini unatumainia chochote kisicho na uhakika, theolojia fulani ya kanisa? Njoo uzaliwe kwa Roho Mtakatifu la sivyo umepotea. Kanisa lako kamwe halitakuokoa, kadiri lilivyo zuri. Kama wewe ni mfuasi tu wa kanisa, umepotea mpaka utakapozaliwa mara ya pili. Njoo! Mungu alitoa Neno kama sauti ya hakika, Yeye hulithibitisha kwa sauti ya hakika, na liko katika utaratibu kikamilifu. Njoo! Kila nafsi iliyokandamizwa na dhambi njoo, mtumainie Bwana. Ninakualika uje. Hakuna mashaka kuhusu hili, Mungu alisema hivyo, Mungu huthibitisha Neno.

<sup>255</sup> Nanyi mnalisikia kwa baadhi ya mara za mwisho, kwa sababu ninaondoka nchini. Wala kamwe hakutakuwako na mwingine uwanjani mpaka nitakapoondoka, BWANA ASEMA HIVI, hakujakuwako, wala hakutakuwako. Njoo wakati ukiweza. Kumbukeni, nitakutana nanyi kwenye Hukumu.

<sup>256</sup> Unasema, “Unapaswa kuimba wimbo wa kusikitisha.” Unapaswa kusimama kutoka kitini mwako, na uje kwa imani, sio kwa wimbo wa kusikitisha, bali Neno la Mungu, na ushuhuda wa Roho Mtakatifu. Ikimbieni ghadhabu ijayo ya Mungu, ikimbieni mioto ya kuzimu iliyo nyuma yenu. Njoo, wakati ukiwa na nafasi ya kuja.

<sup>257</sup> Kumbukeni, ninasema katika Jina la Yesu Kristo: Sitawajibika kwa dhambi zako kwenye ile Siku ya Hukumu kama hutakuja sasa hivi na kumpokea Kristo.

<sup>258</sup> Wewe ambaye huna Roho Mtakatifu, wewe ambaye hujui kwamba wewe ni Mkristo halisi, njoo, ninakupa changamoto, ninakuita, ninakushawishi, katika Jina la Yesu Kristo uje. Unafikiri ni mbali sana na roshani? Itakuwa ni umbali zaidi ya hapo, utakapotembea kwenye barabara hiyo kuelekea kuzimu ya Milele, ambapo utaungua wakati fulani Milele.

<sup>259</sup> Ee Bwana, yaliyosalia ni Yako, siwezi kufanya zaidi.

<sup>260</sup> Saa inachelewa, subira ya Mungu inazidi kupungua. Huenda huu ukawa ndio wakati wa mwisho utakaopata kuwa na wito moyoni mwako, afadhali uje. Huenda ukaulilia wito huo usiku fulani wakati umelala huko nje kwenye barabara kuu, damu ikitoka kwenye mishipa yako, umebanwa chini ya gari;



umelala pale kitandani, naye daktari akisema umekwisha, huenda ukataka hisia hiyo ije moyoni mwako, haitakuwepo, Yeye atakucheka. Afadhali uje sasa. Kumbukeni, nawaambia, katika Jina la Bwana.

<sup>261</sup> Wewe amini...Sijajiita mwenyewe nabii Wake, mliniita. Ninajua Neno la Bwana basi, ni kweli, Yeye amelithibitisha. Njoo.

<sup>262</sup> Njoo kila nafsi, njoo. Hiyo ni kweli, njoo, njoo sasa, wakati unapoweza kuja. Ikimbieni hasira ijayo, kufuatia haya.

Mwokozi,

Vema, wafanyakazi wa binafsi, njoni.

. . . kilio changu kinyenyekevu;

Unapozuru wengine,

Mwenye dhambi, njoo pamoja nao.

. . . usinipite . . .

Unasema, unaogopa kupoteza usingizi kidogo? Vipi kuhusu Uzima?

Mwokozi, Mwokozi, (. . . ? . . .)

Usinipite.

Mwokozi, Mwokozi,

Sikia kilio changu kinyenyekevu;

Wakati . . .

<sup>263</sup> Dakika moja tu. Ninyi wanafunzi wa Kimethodisti hapa, ningependa kuzungumza nanyi kwa muda kidogo tu. Aliyepiga magoti hapa mbele yangu ni mhubiri wa Kimethodisti, ndugu yake ni mmoja wa watu mashuhuri huko Asbury. Angali Mmethodisti, bali amejazwa na Roho Mtakatifu. Nguvu za Mungu ziko maishani mwake.

<sup>264</sup> Ndugu Collins, waweza kusimama tu kwa miguu yako, kwa dakika moja? Mhubiri wa Kimethodisti, hii hapa familia yake wote ni Wamethodisti, alipitia kwenye chuo cha Kimethodisti, na shule, kila kitu, digrii za juu, na kadhalika, naye huyu hapa. Akaisikia Sauti ya Mungu, na akaja, na akapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ni halisi, Ndugu Collins? kwa wanafunzi wa Kimethodisti.

<sup>265</sup> Njoni nyote. "Kuna Chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli." Njoni.

Loo, sikia kilio changu kinyenyekevu;

Unapozuru wengine,

Usinipite.

<sup>266</sup> Sasa hebu sote tuinamishe vichwa vyetu kila mahali. Wamethodisti, ninyi ombeni jinsi mnavyoomba katika kanisa lenu la Kimethodisti; Wabaptisti, fanyeni vivyo hivyo; Mpresbiteri, fanya vivyo hivyo; Wapentekoste, fanyeni vivyo

hivyo. Ninyi hapa mliopiga magoti, ninawakabidhi kwa Yesu Kristo kama nyara za Neno Lake.

<sup>267</sup> Baba yetu wa Mbinguni, ninakupa Wewe kundi hili la watu, usiku wa leo, kama nyara za Ujumbe Wako, wa Roho Wako Mtakatifu, sauti ya hakika inayotokea inayothibitisha kwamba Wewe hujafa, bali Wewe ni Kristo aliye hai, unayeishi katika Kanisa Lako, unayeishi ndani ya watu Wako, unayewapa Roho Mtakatifu, ukinalika nije, kwa wote watakaokuja, bila kujali ushirika wao, na mfumo wao ambao huenda wao ni wafuasi wake.


<sup>268</sup> Wewe ni Mungu, hubadiliki, unajithibitisha Mwenyewe kuwa Mungu, unajua moyo wa kila mtu, unajua jina la kila mtu, unajua hali yao, upumbavu wao, unajua kila kitu, Mungu, kwa sababu Wewe ni Mungu aliye kila mahali, mwenye nguvu zote, asiye na kikomo.

<sup>269</sup> Ninaomba ya kwamba utawaokoa, Bwana, kwa neema yako, uwajaze na Roho Mtakatifu, mtume Roho wa Mungu juu ya kusanyiko hili lote, Bwana, na jalia tu kila moyo uloweshwe. Jalia waaminio sasa wapakwe mafuta na Roho Mtakatifu, wapate kumshukuru Mungu kwamba wameokoka katika siku hizi, tujalie, Bwana, jalia kila mtu aliyekandamizwa na dhambi.

Nitawaacha wahudumu waje hapa nje, nitawasukuma hapa, msimame juu ya hawa ndugu hapa . . . ? . . .

Vema, Ndugu, nimechoka na nimedhoofika. Utachukua ibada? Mungu akubariki . . . ? . . .

(Shukeni kati yao. Shukeni hapa chini.)

<sup>270</sup> Sasa hivi, hii ndiyo saa. Amina. Simama kwa miguu yako upate kumpokea Roho Mtakatifu, kila mmoja wenu. 

61-0415E Sauti Isiyojulikana  
Illinois Wesleyan University  
Bloomington, Illinois Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)